JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

# MWONGOZO WA MAADILI NA UTAMADUNI WA MTANZANIA

CS CamScanner

# VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| **UNESCO** | Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Elimu, Sayansi na Utamaduni |
| **BASATA** | Baraza la Sanaa la Taifa |
| **BFT** | Bodi ya Ukaguzi wa Filamu na Michezo ya Kuigiza |
| **TaSUBa** | Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo |
| **BMT** | Baraza la Michezo la Taifa |
| **BAKITA** | Baraza la Kiswahili la Taifa |
| **TCRA** | Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania |
| **TET** | Taasisi ya Elimu Tanzania |
| **JAMAFEST** | Tamasha la Utamaduni na Sanaa la Jumuiya ya Afrika Mashariki |
| **AZAM MEDIA** | Shirika la Utangazaji la AZAM |
| **VPL VODACOM** | Shirika la Mawasiliano ya mkononi la Vodacom |



CamScanner



Mhe. Samia Suluhu Hassan
**RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# UJUMBE WA MHE. RAIS

***"Taifa letu limejengwa kwa misingi inayozingatia utamaduni, mila na desturi zetu".***

Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika nyakati tofauti amekuwa akizungumzia kwa msisitizo suala la mmomonyoko wa maadili hususan kwa vijana kutowaheshimu wakubwa, vitendo viovu, mavazi yasiyo na staha, lugha chafu, n.k. Pia, amekuwa akizungumzia suala la maadili ya wasanii na kuwasisitizia wawe kioo cha jamii kwa kuishi maisha yenye maadili yanayoendana na mila na desturi za Mtanzania. Kuandaliwa kwa Kitabu hiki ni utekelezaji wa maono ya Mheshimiwa Rais, ambaye ameliona janga la mmomonyoko wa maadili kuwa ni kikwazo kikubwa cha maendeleo endelevu yaTaifa letu.
Katika kuelezea hayo, Mheshimiwa Rais amesema,

"Lakini Tanzania tujiulize, ukiangalia mfumo wa Skauti, mfumo wa vijana wa umoja wa Chama cha Mapinduzi, Umoja wa Vijana wa vyama mbalimbali vya siasa na Girl Guides wetu, tujiulize ukosefu wa maadili na vitendo viovu unatoka wapi Tanzania?".



CamScanner

“Tukiwa tuna taasisi zote hizi zenye mifumo mikubwa lakini bado tuna idadi kubwa ya vijana wanaopotoka, tujiulize tunakwama wapi? Tumekosea wapi? Na hilo swali naliacha kwa taasisi zote nilizozitaja hapa”.

Swali analoliuliza Mheshimiwa Rais linatuhusu sote katika nyanja mbalimbali za maisha yetu, familia, malezi ya watoto na vijana wetu, katika maeneo yetu ya kazi na katika shughuli zote za kijamii na za kitaifa kwa ujumla.

Kitabu hiki kinafungua njia ya kupambana na janga hili la mmomonyoko wa maadili. Aidha, ni kichokoo tu cha kuanzishwa kwa mjadala mpana wa kitaifa, ambapo sisi sote tutaweza kutafakari kwa kina namna ya kukabiliana na janga hili, ili kujenga Taifa bora kwa maono ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.



CamScanner



Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa
**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**

# UJUMBE WA MHE. WAZIRI

Tangu enzi za mababu na mabibi zetu utamaduni umekuwa kiungo muhimu kwa jamii katika kuadilisha, kuelimisha, kuburudisha na kukemea vitendo viovu na kutunza Maadili, mila na desturi za Mtanzania. Mambo haya yaliweza kurithishwa na kuendelezwa kama yalivyokusudiwa. Hata hivyo, katika kipindi cha karne ya 19 baada ya kuja kwa wakoloni masuala mengi yalianza kubadilika kutokana na mfumo wa kikoloni ambao uliwataka Waafrika kubadilisha mitazamo katika nyanja za kiuchumi, siasa na kijamii - utamaduni.

Mifumo hiyo iliwataka Waafrika kufuata matakwa ya wakoloni hao kwa minajili ya kuendeleza utamaduni wao na kuufifisha Utamaduni wa Mwafrika. Wakoloni walibeza Utamaduni wa Kiafrika kwa madai kuwa ni wa kishenzi, duni na hauna manufaa yoyote. Dhana hiyo ilijengeka kiasi cha kuwafanya baadhi ya Waafrika kuanza kudharau, kupuuza na kubeza misingi ya asili na mazingira ya Kiafrika ikiwamo Maadili, mila na desturi za Watanzania.

Matokeo ya dhana hiyo, yamesababisha kuzuka kwa wimbi kubwa la mmomonyoko wa Maadili katika jamii unaotokana na baadhi ya wanajamii kutozingatia mila na desturi za Watanzania, malezi na makuzi yasiyozingatia asili na mazingira ya Kitanzania na kuiga mitindo ya maisha ya tamaduni za kigeni, uvaaji, uchezaji wa muziki, n.k. kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.



CamScanner

Katika kukabiliana na changamoto hii, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa taasisi za dini, mashirika ya umma na watu binafsi imeendelea kutoa elimu kuhusu umuhimu wa kuzingatia Maadili ya Mtanzania kwa kuratibu na kuendesha vikao, mikutano, kampeni, uwasilishaji wa mada mbalimbali zinazohusu kuenzi, kulinda, kurithisha na kuendeleza Maadili ya Mtanzania kupitia vyombo vya habari.

Sanjari na jitahada hizo, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ambayo ni msimamizi na mratibu wa shughuli zote zinazohusu maendeleo ya utamaduni, imeamua kuandaa *Kitabu cha Utamaduni na Maadili ya Mtanzania* ili kulinusuru Taifa dhidi ya mmomonyoko wa Maadili. Kitabu hiki kinalenga kutoa mwongozo kwa jamii ya Kitanzania ili kurejea katika misingi yetu ya Maadili kama Taifa kwa kupenda, kuthamini na kuheshimu mila na desturi zetu ambazo ni miongoni mwa nguzo kuu za utamaduni wetu. Aidha, kitabu hiki kinazingatia tamko la *Sera ya Utamaduni la mwaka 1997, Sura ya Pili, Kipengele cha Pili, Sehemu ya Tatu (2:2:3) kuwa tuna wajibu wa kurithisha na kuendeleza Maadili, Mila, na Desturi Nzuri*.

Pia, kitabu hiki kinakusudia kutoa mwelekeo na umuhimu wa kuzingatia Maadili kwa makundi mbalimbali ya jamii wakiwamo wanafunzi katika ngazi mbalimbali za elimu, vijana, watumishi wa umma na jamii kwa ujumla. Vilevile, kitabu hiki, kitatambua na kusisitiza umuhimu wa kuzingatia Sheria, Kanuni, na Miongozo mbalimbali inayosimamia Maadili katika ngazi au kada mbalimbali zikiwamo za utumishi wa umma na jamii kwa ujumla.

Hali kadhalika, kitabu hiki kina Sura Tano, ambapo Sura ya Kwanza imejikita katika Usuli; Sura ya Pili Mmomonyoko wa Maadili katika Jamii; Sura ya Tatu Wajibu wa Makundi Mbalimbali katika Kukuza na Kuendeleza Utamaduni na Maadili; Sura ya Nne Usimamizi, Uhifadhi, Utekelezaji na Uendelezaji wa Utamaduni na Maadili na Sura ya Tano Mambo Muhimu ya Kuzingatia/ Mapendekezo.

Ni matumaini yangu kuwa kitabu hiki kitatumika kama nyezo muhimu katika kulirejesha taifa kwenye misingi ya Maadili yetu. Aidha, kitasaidia kulinusuru Taifa la Tanzania kutoka katika minyororo ya tamaduni za kigeni na kujenga moyo wa kuthamini, kudumisha na kuendeleza Maadili mema kwa jamii ya Watanzania.

Mhe. Mohammed Omar Mchengerwa
**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**



CS CamScanner



Dkt. Hassan Said Abbasi
**Katibu Mkuu**
**WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**

# DIBAJI

Kitabu hiki kinaeleza juhudi za Serikali za kukuza na kujenga Maadili na Utamaduni wa Mtanzania. Uhai na utambulisho wa Taifa lolote duniani, hutegemea utamaduni wa Taifa hilo. Kwa maneno mengine, utamaduni ni kielelezo na utambulisho wa Taifa na watu wake. Baba wa Taifa Hayati Mwalimu J.K. Nyerere aliwahi kusema, 'Taifa lisilokuwa na utamaduni wake ni sawa naTaifa mfu; ni sawa na mtu bila kuwa na roho' (1962). Maneno hayo ya busara yanaweka msingi kuwa uhai wa Taifa na utashi wa watu wake, unategemea utamaduni wa Taifa hilo. Pia, imebainika kuwa chimbuko la mwenendo mwema katika maisha ya kila siku ni zao halisi la utamaduni wa jamii husika mathalani, kuishi kwa kufuata Maadili, miiko, mila na desturi za jamii husika. Aidha, mwenendo mwema ni jambo la msingi sana na ni lazima utiliwe maanani katika kila nyanja ya maisha ili kulinda utambulisho wetu.

Hivi sasa, kumekuwapo na viashirio vya kuporomoka kwa Maadili yetu kama Taifa kwa kuendekeza tabia ya kuiga tamaduni za kigeni ambazo kimsingi zinakinzana na tamaduni zetu. Imekuwa jambo la kawaida kwa vijana na watoto wadogo kutoheshimu wakubwa, kujihusisha na biashara haramu kama vile; Dawa za kulevya, ukahaba, ubakaji, uhusiano wa mapenzi wa jinsia moja, mimba za utotoni, utoaji wa mimba, mauaji ya vikongwe; na yale ya watu wenye ulemavu wa ngozi, kutupa watoto wachanga, lugha za matusi, rushwa, ujambazi, wizi, uvivu na uvaaji wa mavazi yasiyo na stara. Kukithiri kwa vitendo hivyo kunachochewa zaidi na matumizi mabaya ya teknolojia na athari za mitandao ya kijamii.



CamScanner

Kitabu hiki kimekusudia kuikumbusha jamii kuwa, thamani yetu inategemea namna tunavyolinda na kuenzi utamaduni wa taifa letu. Hivyo basi, tuna wajibu wa kushiriki kikamilifu katika juhudi hizi ili kulinusuru taifa na mmomonyoko wa Maadili ambao umekuwa ukiongozeka siku hadi siku kwa kisingizio cha utandawazi. Kadhalika, kitasaidia jamii kujitambua na kuelekeza jitihada za makusudi katika kuheshimu na kulinda utamaduni na Maadili yetu. Vilevile, maudhui yake yanahamasisha makundi mbalimbali ya jamii kushiriki kikamilifu katika mikakati iliyopo ya kujenga na kuimarisha misingi ya Maadili na Utamaduni wa Mtanzania, makundi hayo ambayo majukumu yao yameanishwa ni pamoja na; Asasi za Kijamii, Bodi mbalimbali za Kitaaluma, Sekta Binafsi, Vyombo vya Habari, Wananchi na Wadau wengine.

Ninatoa rai kwa wadau wote, kusimama imara ili kutetea utamaduni na Maadili yetu kwa nguvu zote. Kila mmoja akitimiza wajibu wake katika nafasi yake, tutaweza kukabiliana na mmomonyoko wa Maadili.



CamScanner

# YALIYOMO

VIFUPISHO VYA MANENO ........................................ ii
UJUMBE WA MHE. WAZIRI ........................................ iii
DIBAJI ........................................ v
YALIYOMO ........................................ vii

SURA YA KWANZA ........................................ 1
UTANGULIZI NA DHANA MSINGI ........................................ 1
1.0 Utangulizi ........................................ 1
1.1 Dhana ya Maadili na Utamaduni ........................................ 2
1.1.1 Maadili ........................................ 2
1.1.2 Misingi ya Maadili ya Mtanzania ........................................ 2
1.1.3 Umuhimu wa Maadili ya Kitaifa ........................................ 3
1.2 Hali ya Maadili kwa Tanzania ........................................ 3
1.3 Maadili ya Mtanzania ........................................ 5
3.1.1 Utamaduni ........................................ 6
1.4 Nguzo za utamaduni ........................................ 7
1.5 Madhumuni ya Mwongozo ........................................ 10
1.6 Majukumu ya Taasisi zilizo chini ya Wizara katika kusimamia Maadili ya Kitaifa na Utamaduni wa Mtanzania ........................................ 10
1.6.1 Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) ........................................ 10
1.6.2 Bodi ya Ukaguzi wa Filamu na Michezo ya Kuigiza (BFT) ..... 11
1.6.3 Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) ........................................ 11
1.6.4 Baraza la Michezo la Taifa (BMT) ........................................ 12
1.6.5 Taasisi wa Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) ......... 12
1.6.6 Hitimisho la Sura ya Kwanza ........................................ 12

SURA YA PILI ........................................ 13
MMOMONYOKO WA MAADILI KATIKA JAMII ........................................ 13
2.0 Mmomonyoko wa Maadili ........................................ 13
2.1 Viashirio vya Mmomonyoko wa Maadili (Kwa Kuzingatia Nguzo za Utamaduni) ........................................ 14
2.2 Athari za Mmomonyoko wa Maadili ........................................ 22
2.4.1 Kupotea kwa nguvukazi ya Taifa ........................................ 23
2.4.2 Kuongezeka kwa umaskini katika jamii ........................................ 23
2.4.3 Kudidimia kwa uchumi ........................................ 23
2.4.4 Kupotea kwa historia, utambulisho asili wa Mila na Desturi za jamii ........................................ 23
2.4.5 Kuongezeka kwa utegemezi na uzururaji ........................................ 24
2.4.6 Kukithiri kwa utovu wa nidhamu ........................................ 24
2.4.7 Ongezeko la ujambazi na kugombea mali ........................................ 24
2.4.8 Kukithiri kwa vitendo vya rushwa ........................................ 25
2.4.9 Kuongezeka kwa mimba za utoto na zisizotarajiwa ............... 25



CamScanner

2.3 Njia za kukabiliana na athari za mmomonyoko wa Maadili ..............26
2.4 Mapendekezo kuhusu udhibiti wa mmomonyoko wa Maadili...........26
2.5 Hitimisho la Sura ya Pili.......................................................................28

**SURA YA TATU ...........................................................................29**
**WAJIBU KWA MAKUNDI MBALIMBALI KATIKA KUKUZA NA KUENDELEZA MAADILI NA UTAMADUNI .......................................29**
3.0 Utangulizi ..........................................................................................29
3.1 Wajibu wa familia ...............................................................................29
3.2 Wajibu wa Serikali ..............................................................................30
3.3 Wajibu wa Sekta binafsi .....................................................................32
3.4 Wajibu wa makundi ya jamii ..............................................................32
3.5 Hitimisho la Sura ya Tatu....................................................................35

**SURA YA NNE ...........................................................................36**
**USIMAMIZI, UHIFADHI, UKUZAJI NA UENDELEZAJI WA MAADILI NA UTAMADUNI ..................................................36**
4.0 Usimamizi wa Maadili.........................................................................36
4.1 Njia za usimamizi, uhifadhi, ukuzaji na uendelezaji Maadili na Utamaduni wa Mtanzania .................................................36
4.1.1 Kuandaa na kuendesha vipindi katika Vyombo vya Habari .............................................................................37
4.1.2 Kufanya vikao, mijadala na makongamano na wadau wa aadili na Utamaduni ..............................................37
4.1.3 Kusambaza Mwongozo wa Maadili na Utamaduni wa Mtanzania ...........................................................................37
4.1.4 Kuandaa programu za utoaji elimu kwa umma kupitia mitandao ya kijamii .......................................................38
4.1.5 Kufanya tathimini endelevu ...................................................38
4.2 Hitimisho la Sura ya Nne.....................................................................38

**SURA YA TANO ...........................................................................39**
**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KATIKA KULINDA, KUKUZA NA KUENDELEZA MAADILI NA UTAMADUNI WA MTANZANIA..................39**
5.0 Wazazi/ Walezi kuwa mfano bora katika Familia ..............................39
5.1 Matumizi sahihi ya teknolojia.............................................................40
5.2 Kila Mtu Kujenga Utamaduni wa Uwajibikaji ....................................41
5.3 Kukemea upotofu wowote wa Maadili unaoibuka katika jamii .........................................................................................42
5.4 Kuheshimu imani za kidini..................................................................42
5.5 Kuwa na marafiki wema .....................................................................43
5.6 Kuepuka masuala ya unyanyasaji......................................................44
5.7 Hitimisho la Sura ya Tano...................................................................44

**MAREJELEO ...........................................................................45**



CamScanner

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI NA DHANA MSINGI

## 1.0 Utangulizi

Mmomonyoko wa Maadili ni moja ya tatizo kubwa linalozikumba nchi nyingi duniani na Tanzania ikiwa mojawapo ya nchi zilizoathirika. Tatizo hili linaathiri nyanja nyingi kama vile siasa, uchumi, utamaduni hususani katika sanaa, mila, desturi na suala zima la maendeleo. Mathalani, Utamaduni wa nchi umeathirika, jambo ambalo linasababisha nyanja nyingine kupata nafasi ya kubadili sura ya Taifa na heshima yake.

Mabadiliko ya sayansi na teknolojia yamebadili mwelekeo wa maisha ya binadamu duniani katika mawasiliano, uzalishaji na usambazaji wa taarifa na kuifanya dunia kuwa kama kijiji kimoja. Mabadiliko hayo, yamesababisha watu hususani vijana kuiga tamaduni za kigeni ikiwamo mitindo ya maisha, uvaaji, uchezaji wa muziki, lugha, n.k.

Aidha, mabadiliko haya yameathiri mfumo mzima wa maisha kwa kigezo cha maendeleo. Jitihada mbalimbali za kutunza na kuenzi utamaduni na kulinda Maadili ya Mtanzania zimekuwa zikifanyika na zinaendelea kufanyika.

Serikali ya Tanzania imechukua hatua na jitihada mbalimbali katika kuenzi na kulinda Maadili na Utamaduni wa Mtanzania. Hatua hizo ni pamoja na kuundwa kwa Wizara yenye dhamana ya Utamaduni mwaka 1962; Kuanzishwa kwa Azimio la Arusha mwaka 1967; Kutungwa kwa S heria ya Baraza la Kiswahili la Taifa ya mwaka 1967; Kutungwa kwa Sheria na kanuni mbalimbali ya Maadili katika utumishi wa umma; Taasisi ya Sanaa na Utamaduni iliyojulikana kama Chuo cha Sanaa cha Bagamoyo mwaka 1972; Bodi ya Ukaguzi wa Filamu na Michezo ya Kuigiza mwaka 1976, kuanzishwa kwa vyombo mbalimbali vya usimamizi kama vile Baraza la Sanaa la Taifa mwaka 1984, kutungwa kwa Sera ya Utamaduni mwaka 1997 pamoja na kuridhia Mikataba ya Ushirikiano ya Kikanda na Kimataifa kama vile Mkataba wa UNESCO wa Kulinda Urithi wa Utamaduni Usioshikika wa Mwaka 2003 na Mkataba wa Kukuzwa na Kuenezwa kwa Uanuai wa Kujieleza Kiutamaduni wa Mwaka 2005. Juhudi hizi zinapaswa kuendelezwa na kupewa msukumo kwa kuandaa na kuboresha nyaraka ambazo zitasaidia kuelimisha, kukumbusha na kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kuzingatia Maadili ya Kitaifa na kuendeleza utamaduni wa Mtanzania.



CamScanner

## 1.1 Dhana ya Maadili na Utamaduni

### 1.1.1 Maadili

Maadili ni tabia njema, misingi, kanuni, na taratibu zinazofuata mienendo inayokubalika katika jamii, ambayo inaongoza uhusiano katika makundi ya jamii husika. Maadili yanamtaka mtu kufanya kitu kilicho sahihi, mahali sahihi na wakati sahihi. Kimsingi, MMaadili ni zao la mila na desturi za utamaduni wa jamii inayohusika.

Dhana ya Maadili imetokana na kuwapo kwa miiko na makatazo katika jamii fulani ambayo yalikuwa na malengo ya kuiunganisha jamii, kudumisha amani na kuepusha madhara kama vile magonjwa, kukosa viungo, vifo n.k; Makatazo hayo yalitofautiana kati ya ukoo au jamii moja na nyingine au kati ya watawala na watawaliwa. Mengi ya makatazo hayo ya enzi hizo hayakuandikwa kutokana kutokuwapo kwa taaluma ya maandishi bali yalirithishwa kutoka kizazi kimoja kwenda kingine kwa njia ya masimulizi.

Hivyo, chimbuko la Maadili ya jamii za leo ni mwendelezo wa makatazo yaliyorithishwa kutoka kizazi kilichopita. Baadhi ya makatazo hayo ndiyo chimbuko la Maadili. Kutokana na mabadiliko ya mfumo wa maisha, baadhi ya makatazo yasiyofaa yameondolewa na yale yanayofaa yanaendelezwa na jamii inahimizwa kuyazingatia. Kwa muktadha huu, yapo Maadili yaliyowekwa kutokana na Mila na Desturi, Sheria na Kanuni.

### 1.1.2 Misingi ya Maadili ya Mtanzania

Ili Maadili yaweze kulindwa ni lazima yafahamike. Maadili hujengwa kwa mtu kupitia hatua mbalimbali ambazo msingi wake mkubwa ni malezi hasa ikizingatiwa kuwa huanzia hatua za awali za makuzi kutoka utotoni hadi uzeeni. Hivyo, familia ndiyo  chombo cha kwanza na muhimu sana chenye wajibu wa malezi yaani hatua za mwanzo za Maadili hufundishwa kuanzia  ngazi ya familia, na baadaye kwenye jamii, taasisi za dini na shuleni. Pia, Maadili huweza kufundishwa kupitia machapisho mbalimbali kama vile; Vitabu, vipeperushi, magazet,.na vyombo vya habari na fani za utamaduni kwa pamoja vina mchango katika kutoa elimu kuhusu Maadili. Vilevile, Maadili huweza kufundishwa kupitia semina na hotuba mbalimbali za viongozi wa dini, siasa na mila. Tanzania kama nchi nyingine duniani, hulinda baadhi ya Maadili kwa sheria mbalimbali. Kwa mfano lugha ya matusi ni kosa la jinai, na Mahakama hutoa adhabu kwa kosa hilo. Sheria ya mitandao huadhibu wale wote wanaorusha  picha za utupu au za ngono kwenye mitandao ya kijamii.



CamScanner

### 1.1.3 Umuhimu wa Maadili ya Kitaifa

Maadili hufanya nchi/Taifa liheshimike, pia mtu kuthaminika ndani na nje ya nchi yake. Maadili huleta amani, upendo, mshikamano, utulivu na uadilifu mahali pa kazi na hivyo kufanya nchi au Taifa kupata maendeleo ya haraka. Umuhimu wa Maadili ulisisitizwa pia katika hotuba ya Mwalimu Nyerere ya mwaka 1962. Baba wa Taifa, Hayati Mwl. Julius Kambarage Nyerere, mnamo Juni 28, 1962, akizungumzia kuhusu Katiba ya Jamhuri ya Tanganyika, alisema hivi, "*… it was impossible to devise a fool proof constitution, and that the only real protection against tyranny is a National Ethic…"* Nyerere: (Uhuru na Umoja u.k. 174). **Hapa Baba wa Taifa anatamka wazi kabisa kuwa Katiba hata iwe nzuri namna gani, bila kuwapo na Maadili ya Kitaifa ni kazi bure! Haki na uhuru wa raia inategemea Maadili ya Taifa lenyewe.**

Mifumo ya kisera iliyopita ilijumuisha viongozi wote, watumishi wa umma na wananchi kwa ujumla. Mifumo iliyopo inagusa makundi fulani ya viongozi na watumishi wa umma na kuiacha jamii pana, hali ambayo inasababisha ombwe katika ujenzi wa Maadili nchini na hivyo kusababisha mmomonyoko wa Maadili katika sehemu hiyo ya jamii iliyoachwa. Sehemu hiyo ya jamii iliyoachwa ina muunganiko mkubwa sana na jamii ya viongozi na watumishi wa umma kama sehemu ya familia, wanafunzi, wafuasi, wapigakura na wapokea huduma.

Hali hii inachangiwa na kutokuwapo kwa misingi jumuishi ya Maadili ya Taifa inayofahamika na kueleweka kwa jamii nzima ya Watanzania. Kila jamii inafuata mila na desturi za jamii inayohusika, ambazo nyingine ni potofu. Hivyo, kuna umuhimu wa kuwa na mwongozo wa kisera utakaoelekeza mambo ambayo ni tunu za Maadili za Taifa ambazo zinapaswa kuzingatiwa na Watanzania wote kama utambulisho wa Utanzania wetu. Mfumo wa Maadili ni vyema ukaendana na mabadiliko ya mfumo wa kisiasa na kiuchumi. Upo umuhimu wa mifumo ya Maadili kuhusisha watu wote wa Tanzania na si kundi la watu wachache.

## 1.2 Hali ya Maadili kwa Tanzania

Kwa miaka iliyopita suala la Maadili na malezi hasa katika jamii lilikuwa ni jukumu la watu wote. Watoto waliweza kuonywa/kukanywa na mtu mzima yeyote ambaye hana uhusiano naye wa kindugu. Watoto na vijana walifundishwa malezi mazuri kupitia hadithi, elimu ya jando na unyago pamoja na shuleni. Kwa upande wa wazazi au walezi walitekeleza jukumu lao la malezi kwa asilimia kubwa; malezi ya watoto haikuwa jukumu kubwa la wasaidizi wa kazi za nyumbani kama ilivyo sasa. Vijana na watoto




CamScanner

waliheshimu watu wote pasipo kujali kama ni ndugu wa kuzaliwa au wa karibu. Hali hii iliweza kuchangiwa na mfumo wa maisha uliokuwa kwa wakati huo kabla na baada ya ukoloni. Mathalani, sera ya Ujamaa Tanzania ililenga kuifanya jamii kuwa moja, ilizalisha waungwana, wenye uzalendo kwa taifa lao, upendo, kuaminiana na utu; Watu ambao hawakuwa na uhusiano wa kindugu waliweza kula yamini (kuchanjiana damu) na kuwa ndugu wa damu.

Mabadiliko mbalimbali yanayotokea Duniani ikiwamo utandawazi kwa namna moja au nyingine yalibadili sura ya Maadili na Utamaduni wa Mtanzania. Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia pia vimechangia mabadiliko ya ustawi wa Maadili na Utamaduni, kwa mfano vijana na watoto kuiga tamaduni za kigeni kupitia runinga, filamu, muziki na mitandao ya kijamii. Pia, baadhi ya wazazi au walezi nao wameonekana kunakili baadhi ya tamaduni za kigeni na kuwarithisha watoto na vijana wao; wazazi kuvaa nguo ambazo hazina stara mbele ya watoto na kinyume chake, sababu kubwa hapa inayosemwa ni kwenda na wakati. Pia, mwingiliano wa jamii moja na nyingine kupitia taasisi za mafunzo kama vile shule, vyuo vya elimu ya juu navyo vimeleta athari katika Maadili na Utamaduni kutokana na mchanganyiko wa jamii mbalimbali zenye tamaduni tofauti. Suala lingine ni miongozo na matamko mbalimbali yanayotolewa na nchi wahisani, wafadhili na mashirika yasiyo ya kiserikali ambayo yameleta athari hasi katika Maadili. Kwa mfano, kuna Shirika moja lisilo la Kiserikali ilikuwa na tangazo kwenye runinga linalohusisha watoto kuchapwa fimbo, tangazo lilisisitiza ‘kupiga ngoma na siyo mtoto’. Kwa namna moja au nyingine tangazo kama hili lina uwezo wa kuwaharibu watoto. Kwa kiasi kikubwa, vyombo vya habari ikiwamo redio, runinga na mitandao ya kijamii vinachangia mabadiliko katika Maadili na Utamaduni.

Tanzania ina utajiri mkubwa wa urithi wa utamaduni kwa kuwa na makabila (jamii) zaidi ya 150 yenye mila, desturi, lugha na historia tofauti. Jamii zote hizi huunganishwa na lugha ya Kiswahili. Mila na Desturi za jamii hizo ambazo huongoza maisha ya kila siku zinahusisha masuala mbalimbali ikiwamo: -

i) Aina ya vyakula na vinywaji vya kiasili vya jamii husika.
ii) Utaratibu wa ndoa na sherehe za harusi.
iii) Vifo na taratibu za mazishi, matanga, mirathi, n.k.
iv) Uaratibu wa kazi, mgawanyo wa madaraka ya kazi, zana za kazi, ushirikiano, nafasi ya jinsia katika uamuzi na mgawanyo wa mavuno.
v) Utambuaji wa nyakati na majira au misimu.
vi) Mavazi, mapambo na urembo.
vii) Silaha za kijadi na utaratibu wa maandalizi ya vita na usuluhishi wake unapohitajika.




***Picha ikionesha mavazi yasiyofaa***

## 1.3 Maadili ya Mtanzania

Maadili ya Mtanzania ni pamoja na:-

- Kuwa na nidhamu
- Tabia njema
- Kuwa na utii
- Kuwa mwaminifu
- Kufanya mambo pasipo kupendelea au kukiuka sheria, kanuni na utaratibu uliowekwa
- Kufanya kazi halali
- Kufanya kazi kwa bidii, kwa haki, bila unyanyasaji au upendeleo
- Kushiriki kazi za kujenga taifa
- Kuhimiza upendo, mshikamano na amani ambayo hutokana na kuelewana, kuvumiliana na kuheshimiana
- Kutokubaguana kwa misingi ya kabila, dini, jinsia au rangi



CamScanner

- Kuthamini elimu na mafunzo
- Kuthamini na kutunza rasilimali za Taifa
- Kutotoa au kupokea rushwa
- Kuthamini utu na kulinda maisha ya watu wengine
- Kukuza demokrasia, uwazi na ukweli katika uendeshaji wa mambo yetu
- Kukuza usawa wa kijinsia
- Kutambua na kuendeleza mila na desturi nzuri kama vile kutambua wakati na mahali pa kila jambo, kutambua haki na wajibu wa kila rika (watoto, vijana na wazee)
- Kusetiri miili yetu kwa nguo kadiri inavyowezekana (Kuvaa mavazi yenye heshima na staha)
- Matumizi ya lugha nzuri
- Kuwa na heshima kwa wakubwa na wadogo
- Kusaidia watu wenye uhitaji
- Kuthamini na kutunza mazingira.

Maadili haya na mengine yamekuwa yakifundishwa kwa njia mbalimbali kupitia:-

- Familia
- Jamii
- Taasisi na jumuiya mbalimbali – (K.m. Shule, Asasi za dini)
- Viongozi (Katika hotuba nk.)
- Machapisho mbalimbali – (vitabu, vipeperushi)
- Fani za utamaduni - na Michezo.

Baadhi ya Maadili ya Taifa letu yanalindwa kisheria maana yamewekwa katika Katiba ya Nchi na kwenye sheria mbalimbali. Baadhi ya Maadili yamewekewa misingi katika Sera za Taifa letu. Ni vigumu kuyalinda Maadili ya Taifa ambayo hayajatungiwa Sheria, kanuni. Kuna umuhimu wa kuwa na utaratibu wa wazi wa kulinda Maadili ya Taifa ili tusibakie kulalamika tu pindi utaratibu huo unapokiukwa.

### 1.3.1 Utamaduni

Dhana ya Utamaduni imeelezwa kwa mitazamo tofauti kwa kuzingatia muktadha wa jamii yenye utamaduni huo. Baadhi ya tafsiri zinaeleza kuwa Utamaduni ni maisha yote ya binadamu na namna anavyokabiliana au kumudu mazingira yake. Kutokana na Sera ya Utamaduni ya mwaka 1997, "Utamaduni ni jumla ya mambo yote yanayobuniwa na jamii ili kukidhi utashi na maendeleo yake. Kwa maneno mengine, utamaduni ni mwenendo wa maisha ya jamii, mtazamo wao wa mambo na taratibu zao za kuendesha maisha zinazowatofautisha wao na jamii nyingine. Utamaduni ndiyo



CamScanner

kitambulisho kikuu cha Taifa na kielelezo cha utashi na uhai wa watu wake". Ndagala (2015) ameeleza dhana ya Utamaduni ni 'kitu kizito ambacho kinajumuisha mwenendo mzima wa maisha ya jamii na vitu vinavyothaminiwa ikiwamo, matendo, ishara na viashirio, taasisi na uhusiano. Kwa kuzingatia tafsiri mbalimbali zilizotolewa, Utamaduni ni mwenendo wa maisha ya kila siku ya jamii na utaratibu wao wa kuendesha mambo katika mazingira yao unaowatofautisha wao na jamii zingine nao hupatikana katika mila, desturi, lugha, sanaa, Maadili, malezi, mafunzo na taasisi zake kama jando na unyago, imani, itikadi na miiko, malikale, maliasili, michezo, mapokeo, historia na shughuli za uzalishaji mali.

## 1.4 Nguzo za utamaduni

Utamaduni unajengwa na nguzo sita ambazo ni Mila, Desturi, Lugha, Sanaa, Michezo na Historia[1]. Nguzo hizo ndizo mihimili ya utamaduni wa Mtanzania. Kwa hiyo, umoja, utulivu, udugu, utu, uzalendo, upendo na mshikamano ambavyo Watanzania tunajivunia vinatokana na utamaduni tuliojijengea.

### i. Mila

Ni mambo halali yaliyokubaliwa kufanyika katika jamii. Kwa lugha nyingine ni sheria na taratibu za jamii zisizoandikwa zinazotokana na malezi na mapokeo ya maarifa na ujuzi kuhusu mambo mbalimbali katika maisha. Aidha, mila ni utaratibu wa maisha, mwenendo na jinsi ya kufanya mambo unaofuatwa na jamii fulani kulingana na historia na utamaduni wao. Kwa kawaida, watu hufunzwa mila kwa umakini katika muda wote wa malezi yao tangu utoto hadi utu uzima. Mfano; jamii za Wasukuma, Wanyakyusa na Wahehe, ni nadra kwa mtoto wa kike kusalimia akiwa amesimama wima.

### ii. Desturi

Ni mwenendo wa maisha uliozoeleka kufanywa na jamii fulani ambapo mwenendo huo ukidumu kwa muda mrefu hugeuka na kuwa mila (sheria ya jamii hiyo). Aidha, desturi hujipambanua kama mazoea ya kila siku. Desturi huelezea namna ambavyo jamii inaendesha mambo yake. Mfano kufanya kazi kwa bidii, kupendelea aina fulani ya vyakula au vinywaji, namna ya uandaaji wa vyakula na namna ya kutumia muda wa mapumziko kama burudani n.k

[1] Sera ya Utamaduni ya Mwaka 1997



CamScanner

### iii. Lugha

Lugha ni chombo kikuu kinachotumiwa katika mawasiliano miongoni mwa jamii au Taifa. Lugha ni zao halisi la utamaduni wa jamii inayohusika. Tanzania ina zaidi ya lugha za kijamii zipatazo 150 ambapo zaidi ya asilimia 95 ya Watanzania wanafahamu na kuzungumza lugha ya Kiswahili. Lugha hutumika kupashana habari na kuwasiliana miongoni mwa makundi yanayotumia lugha hiyo. Aidha, lugha ni silaha kubwa inayoweza kutumika kuleta au kuvunja amani. Hivyo, lugha ni nguzo kuu ya utamaduni wa jamii husika inayotumika kuitambulisha, kurithisha mila, desturi, miiko, Maadili, maarifa na utaifa. Yaani lugha ndiyo inayotumika kufasili mihimili mingine ya Utamaduni wa Mtanzania.

### iv. Sanaa

Sanaa ni ustadi wa kuweka na kupanga fikira kwa njia ya hisia au zana. Sanaa huambatana na ufundi, elimu na mafunzo; ni uzuri unaojitokeza katika umbo lililosanifiwa. Mchango wa Sanaa katika Utamaduni ni kuchochea maendeleo ili kukidhi mahitaji ya jamii. Sanaa inaweza kuonekana kwenye vitu, namna ya kuuchezesha viungo vya mwili kwa kufuata mirindimo, miondoko, utoaji wa sauti, uzungumzaji au uandishi wenye mpangilio maalumu ukiwa na lengo la kutoa ujumbe, kuelimisha, kuburudisha na kuhamasisha jambo fulani. Sanaa zimegawanyika katika sehemu kuu tatu ambazo ni sanaa za ufundi, sanaa za maonyesho na sanaa ghibu au za muziki. Sanaa za ufundi hujumuisha uchoraji wa picha, ufinyanzi, ususi na ufumaji; Sanaa za maonesho hujumuisha michezo ya kuigiza ya jukwaani na ngoma za asili. Kwa upande wa Sanaa ya muziki hujumuisha muziki wa asili na muziki wa kisasa.

### v. Michezo

Michezo ni chombo cha kutoa burudani, kujenga na kukomaza afya ya mwili na akili; kwa sasa imeonekana ni sehemu ya ajira na chanzo cha mapato kwa mtu mmojammoja na taifa kwa ujumla. Aidha, hujenga nidhamu, uhusiano, ushirikiano, kuibua na kutangaza vipaji hususani nchi inaposhiriki katika michezo ya kimataifa na kulitambulisha taifa husika.

Jamii za Kitanzania zilikuwa zikishiriki michezo katika maeneo yao, baadhi ya michezo ni mieleka, kulenga shabaha kwa upinde na mishale, kirumbizi bao, rede, pia, mdako, kuruka kamba, kuogelea, n.k. Michezo hii ilijenga ari ya kujiamini na kuwa utambulisho wa jamii. Michezo hii hujulikana kama michezo ya jadi. Kutokana na mwingiliano wa tamaduni mbalimbali, michezo hii ilififia na badala yake michezo mipya iliingizwa kutoka ughaibuni ikiwamo mpira wa miguu, netiboli, ndondi, mpira wa meza, mpira wa mikono, mbio za



CamScanner

baiskeli n.k. Kwa sasa, michezo mbalimbali na imekuwa chombo cha kutoa burudani, ni chanzo cha kuzalisha ajira, na kuchangia katika pato la mtu mmojammoja na kuongeza pato la Taifa.

**vi. Historia**

Ni kumbukumbu, matukio au taarifa kuhusu mambo yaliyofanywa wakati uliopita katika jamii. Taarifa za mambo hayo zinaweza kuwa nzuri au mbaya. Kimsingi, historia huonesha chimbuko au asili ya jamii fulani na mazingira halisi yaliyokuwapo kwa wakati huo na namna jamii hiyo ilivyoweza kupambana katika kukidhi mahitaji yake ya kila siku. Hivyo, ili kujenga utamaduni halisi wenye kuleta maendeleo kwa wananchi ni vyema kuanza na utafiti wa historia na mazingira ya jamii husika. Historia huelezea maisha ya jamii kwa kipindi kilichopita na huonesha dira ya maisha kwa siku za usoni. Mifano ya matukio ya kihistoria yaliyowahi kutokea katika nchi yetu ni pamoja na; Vita vya Maji Maji (1905-1907); Uhuru wa Tanganyika Mwaka 1961, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964, Mapinduzi ya Zanzibar mwaka 1964, Janga la Njaa la Mwaka 1974, Vita vya Kagera (Mwaka 1978-1979); Tanzania kuingia kwenye Mfumo wa Vyama vingi vya Siasa Mwaka 1992, Uchaguzi wa Kwanza wa Vyama vingi vya Siasa nchini Tanzania Mwaka 1995; Tanzania kuingia katika Uchumi wa Kati Mwaka 2020, na mengine mengi.




***Picha ikionesha nguzo muhimu za utamaduni***



CamScanner

## 1.5 Madhumuni ya Mwongozo

Madhumuni ya Mwongozo huu ni:-

- Kutoa dira kwa jamii kuhusu umuhimu wa kuzingatia na kuheshimu Maadili ya Mtanzania; kuelimisha jamii kuzingatia misingi ya Maadili ya kitaifa na utamaduni wa Mtanzania;
- Kukuza uelewa wa Watanzania katika makundi mbalimbali ya jamii kufuata na kuishi kwa kuzingatia mila, desturi na miiko ambayo ndiyo misingi ya Maadili ya kitaifa na utamaduni wa Mtanzania;
- Kutekeleza dhamira ya kukabiliana na janga la mmomonyoko wa Maadili kwa jamii ya Watanzania;
- Kushirikisha familia na jamii katika ujenzi wa Maadili katika kaya na maeneo yao;
- Kuimarisha upatikanaji wa fursa za elimu ya Maadili katika ngazi zote za elimu;
- Kuendeleza utamaduni wa Mtanzania katika ukuzaji na usimamizi wa Maadili nchini;
- Kuhamasisha uzalendo, uadilifu, uwajibikaji na uwazi kama nguzo muhimu za utawala bora kwa kuimarisha mifumo na vyombo vya kusimamia masuala ya Maadili na utawala bora nchini.

## 1.6 Majukumu ya Taasisi zilizo chini ya Wizara katika kusimamia

**Maadili ya Kitaifa na Utamaduni wa Mtanzania**

Wizara yenye dhamana ya utamaduni ndiyo yenye jukumu la kusimamia utamaduni na Maadili ya jamii nchini kupitia taasisi zilizo chini yake. Taasisi hizo ni Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA); Bodi ya Ukaguzi wa Filamu na Michezo ya Kuigiza (BFT); Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa); Baraza la Michezo la Taifa (BMT); na Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA). Aidha, Taasisi hizi hufanya kazi kwa karibu na Vyama na Mashirikisho ya wadau. Majukumu ya Taasisi hizo ni kama ifuatavyo:

### 1.6.1 Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA)

Ni Taasisi ya Umma iliyoundwa kwa Sheria ya Bunge Na. 23 ya Mwaka 1984 kwa lengo la kusimamia maendeleo ya Sanaa nchini. Pamoja na majukumu mengine, Baraza linatekeleza majukumu yafuatayo:

- Kutoa ushauri na kuchukua hatua pale inapobidi kwa wasanii wanapokiuka sheria, taratibu na kanuni;
- Kushirikiana na Kamati ya Maudhui ya TCRA kutoa elimu kwa wasanii na wadau wa Sanaa;



CS CamScanner

- Kuhimiza ukuzaji wa utamaduni halisi wa Sanaa ya Kitanzania;
- Kudumisha ubobezi na ubora wa hali ya juu wa kazi za Sanaa na ubunifu; na
- Kuhimiza ubunifu na uvumbuzi wa kazi za Sanaa.

### 1.6.2 Bodi ya Ukaguzi wa Filamu na Michezo ya Kuigiza (BFT)

Bodi ya Ukaguzi wa Filamu na Michezo ya Kuigiza (BFT) ni taasisi ya Serikali iliyoanzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 4 ya Mwaka 1976 kwa lengo la kulinda utamaduni kwa kuhakikisha kuwa sanaa ya filamu na michezo ya kuigiza inazingatia Maadili ya Mtanzania. Sheria na Kanuni za Bodi ya Filamu zimejikita katika kuangalia mwenendo wa Maadili kwa waigizaji na wadau wa Filamu na Michezo ya Kuigiza. Katika kulinda Maadili hayo, Bodi inatekeleza yafuatayo:

- Kukagua filamu zote na kutoa vibali vya kuoneshwa hadharani;
- Kutoa vibali vya utengenezaji wa Filamu kwa watengenzaji kutoka nje ya nchi na kusimamia utengenezaji wa filamu hizo;
- Kukagua na kutoa leseni za majumba ya sinema nchini;
- Kusimamia na kuratibu utendaji wa asasi zinazojishughulisha na masuala ya filamu nchini; na
- Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sheria ya filamu na kanuni zake.

### 1.6.3 Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA)

Ni chombo cha Serikali kilichoundwa kwa Sheria ya Bunge Na. 27 ya Mwaka 1967 kwa lengo kuratibu na kusimamia asasi na mawakala wote wanaokuza Kiswahili katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kama tunavyofahamu, lugha ni kipengele muhimu sana katika kukuza Maadili ya jamii. Pia, Lugha ni njia ya kupitishia na kurithisha Maadili ya jamii yoyote ile. Baraza lina nafasi kubwa katika kujenga, kuhifadhi na kurithisha Maadili ya jamii ya Watanzania. Hivyo basi, pamoja na mambo mengine, Baraza hutekeleza majukumu yafuatayo:

- Kutoa elimu kuhusu matumizi ya lugha sahihi kupitia vyombo mbalimbali vya habari mfano magazeti, redio na televisheni kuhusu matumizi fasaha na sanifu ya lugha ya Kiswahili. Aidha, kukemea upotoshaji wa lugha na kuelekeza namna nzuri ya utumiaji wa lugha kwa kufanya masahihisho ya makosa katika matumizi yanayohusisha utumiaji wa lugha isiyo fasaha.
- Kuandaa makala mbalimbali katika magazeti ya kila siku ili kutoa fursa kwa jamii kujifunza makosa mbalimbali yanayofanywa katika matumizi ya lugha ya Kiswahili;



CamScanner

### 1.6.4 Baraza la Michezo la Taifa (BMT)

Baraza la Michezo la Taifa (BMT) ni Taasisi ya Serikali iliyoundwa kwa Sheria ya Bunge Na. 12 ya Mwaka 1967 pamoja na marekebisho yake katika Sheria Na. 6 ya mwaka 1971 kwa lengo la kuendeleza michezo nchini kwa kushirikiana na vyama vya michezo na kulinda Maadili ya kitanzania katika sekta ya Michezo. Majukumu yake ni pamoja na:-

Kusimamia na kuratibu uundwaji wa Kamati ndogondogo za Nidhamu, Usuluhishi na Rufaa katika mashirikisho na vyama vya michezo nchini;

- Kupokea na kujadili rufaa au malalamiko kuhusu masuala ya michezo mbalimbali kutoka katika vilabu, vyama, wanamichezo, waamuzi, walimu wa Michezo, madaktari na viongozi wa timu;
- Kupitia na kuchambua vielelezo ikiwa ni pamoja na Kanuni na Sheria za Michezo husika;
- Kutoa uamuzi kuhusu mabadiliko au rufaa mbalimbali zinazowasilishwa; na
- Kuandaa mafunzo kwa viongozi wa Vyama na Vilabu vya Michezo.

### 1.6.5 Taasisi wa Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa)

Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBA) ilianzishwa rasmi kama Wakala wa Serikali kwa Tangazo la Serikali Na. 220 la tarehe 2 Novemba, 2007 chini ya Sheria ya uanzishwaji wa Wakala wa Serikali. Taasisi hii ilianzishwa ili kukuza, kuhifadhi na kuendeleza Sanaa na Utamaduni nchini. Majukumu ya Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo ni kama yafuatayo:-

- Kutoa programu za mafunzo yenye ubora wa hali ya juu katika uzalishaji wa Makala jongefu, Sanaa na Utamaduni;
- Kutoa ushauri wa kitaalamu na tafiti katika masuala yanayohusu Sanaa na Utamaduni; na
- Kuwezesha utawala Bora katika usimamizi wa rasilimali za Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo.

### 1.6.6 Hitimisho la Sura ya Kwanza

Katika kuendeleza jitihada za kuwa na Maadili mema nchini, ni muhimu kuendelea kuchukua hatua madhubuti za kupambana na hali ya mazingira ambayo yanaweza kusababisha mmomonyoko wa Maadili katika Taifa letu. Mojawapo ya masuala muhimu katika kuendeleza vita hii ni kuendelea kuzingatiwa kwa mila, desturi na Utamamduni wa Mtanzania kwani ndiyo msingi mkubwa katika ujenzi wa taifa lenye Maadili mema.



CamScanner

# SURA YA PILI
# MMOMONYOKO WA MAADILI KATIKA JAMII

Dunia inakwenda kasi sana kutokana na kuchangamana kwa jamii mbalimbali duniani na maendeleo ya Sayansi na Teknolojia. Hali hii imesababishwa na mambo mengi ikiwapo mwingiliano wa watu kupitia mitandao ya kijamii, kukua na kuenea kwa miji. Watu hasa viijana wameamua kurithi kila kitu bila mipaka kutokana na ukweli kuwa vijana ni kizazi cha kuiga na kunukuu kila kitu. Katika sura hii, tutaangalia zaidi mmomonyoko wa Maadili katika jamii, athari zake kwa jamii na namna ya kupambana na hali hii katika jamii.

## 2.0 Mmomonyoko wa Maadili

Ni ukiukwaji wa tabia njema, misingi, kanuni, na mienendo inayokubalika katika jamii. Ni hali inayojidhihirisha kupitia vitendo na mienendo iliyo kinyume na misingi inayokubalika au kuwekwa na jamii katika kuendesha maisha ya kila siku. Aidha, mienendo hii hujidhihirisha katika nyanja kama vile lugha, mavazi, malezi, huduma za jamii kama vile hospitali, mahakamani shuleni na uhusiano wa kijamii. Kimsingi, Maadili mema hutokana na mila na desturi za utamaduni wa jamii inayohusika.

## 2.1 Viashirio vya Mmomonyoko wa Maadili (Kwa Kuzingatia Nguzo za Utamaduni)

Tatizo la mmomonyoko wa Maadili linazikumba nchi nyingi duniani na Tanzania ikiwa mojawapo. Ukubwa wa tatizo unatofautiana kutoka nchi moja hadi nyingine kulingana na mifumo ya udhibiti iliyopo, mikakati ya kukabiliana, utayari wa jamii husika na utashi wa viongozi. Kutokana na mmomonyoko wa Maadili nyanja mbalimbali zimekumbwa na athari hizo ukiwamo Utamaduni wa Taifa. Pamoja na jitihada mbalimbali zilizofanyika ili kukabiliana na tatizo hilo, bado jamii ya Kitanzania imeendelea kukabiliwa na tatizo hili ambalo linakuwa kwa kasi kutokana na mabadiliko mbalimbali ya mfumo wa maisha ikiwamo sayansi na teknolojia.

Viashirio vya mmomonyoko wa Maadili kwa kuzingatia Utamaduni wa Mtanzania ni hivi vifuatavyo;-



CamScanner

### a) Lugha

Lugha ni kiungo kikubwa sana katika kulinda au kupotosha Maadili kuendana na matumizi yanayohusika. Maadili ya Mtanzania, huwataka wazungumzaji kutumia lugha sahihi na fasaha kwa wakati na muktadhasahihi, na sio kutumia lugha ya matusi na kejeli ambayo husababisha ugomvi, kuvunjika kwa amani, vita, au kuleta uhusiano mbaya kati ya mtu na mtu, taifa na mataifa, na kurudisha nyuma maendeleo ya nchi yetu, kwani bila amani hakuna kazi yoyote itakayofanyika. Mtu anaweza kuonekana ni mwenye Maadili kutokana na matumizi yake ya lugha kimsamiati, kimuundo na kimisemo kwa kuzingatia rika, matabaka na mazingira yanayomzunguka mzungumzaji.

Hata hivyo, nchi imeendelea kushuhudia lugha ikitumika kama kichocheo cha uvunjifu wa Maadili katika marika yote za mwanadamu kwa mfano maneno yasiyokuwa na staha mbele ya halaiki, watoto, au watu wa rika tofauti. Baadhi ya maneno yanalazimika kutanguliwa na maneno mengine ili kupunguza ukali na kulinda heshima ya mtamkaji, mathalani neno 'ashakum', hutumika kuomba radhi kwa mtu au watu kabla ya kuzungumza jambo ambalo linaweza kumuudhi mlengwa au mtu yeyote anayesikia kinachotamkwa. Kwa mfano neno **busha** au **mabusha** kwa Maadili yetu si neno linaloweza Maadili kutamkwa hadharani kwani linadhalilisha au kukera wengine; ili kulipunguza ukali au ukakasi katika masikio ya wasikilizaji neno **'ngirimaji'** hutumika badala yake. Maneno mengine ni kama **'kuzaa'** badala ya **'kujifungua'** au **kupata mtoto**; **'kukojoa'** badala ya **'kwenda haja ndogo'**; **'kunya'** badala ya '**kwenda haja kubwa**', **'kujamba'** badala ya **'kupumua au kushuta'**, **mimba** badala ya **'ujauzito'** na kadhalika. Matumizi ya lugha za matusi ni jambo linaloonesha kutoweka kwa Maadili katika jamii.

Nchini Tanzania, jamii imekuwa ikichangia mmomonyoko wa Maadili kwa kuzungumza maneno ambayo hayafai kusikika h adharani ambapo imechangia baadhi ya watu kuchukuliwa hatua na vyombo vya sheria kama jedwali linavyoonesha takwimu za Jeshi la Polisi nchini, takwimu za mwaka 2016-2018 kuna matumizi ya lugha ya matusi kama inavyoonesha katika jedwali hili. Aidha, takwimu hizi zinaonesha visa vilivyoripotiwa tu. Hivyo, tatizo ni kubwa kuliko inavyoonekana katika takwimu.



CamScanner

**Jedwali Na. 1: Lugha ya matusi**

| Na. | 2016 | 2017 | 2018 |
|---|---|---|---|
| 1. | Lugha ya matusi (3,471) | Lugha ya matusi (4,841) | Lugha ya matusi (4,973) |

### b) Mmomonyoko wa Mila na Desturi

Mila na Desturi zimebeba hazina kubwa ya Maadili ya Mtanzania, na hizi zikifuatwa bila kuvunjwa itakuwa kinga ya mmomonyoko wa Maadili katika nchi yetu. Kwa kuwa ndiyo msingi mkubwa wa Utamaduni ambao umejengeka katika akili, fikira, imani na maarifa ambayo huongoza maisha ya jamii husika kihistoria, kijiografia na kiuchumi.

Baadhi ya mila na desturi za jamii zinahimiza kulinda rasilimali na mali za nchi; kutunza mazingira, kujenga usawa wa kijinsia; kuthamini na kufanya kazi kwa bidii, kusaidia watu wenye mahitaji; kuwa na heshima kwa wakubwa na wadogo, kuvaa mavazi ya kusitiri milli, n.k.

Kwa sasa kumekuwa na ukiukwaji mkubwa wa Maadili katika Taifa letu kutokana na kupuuza, kudharau na kubeza vipengele vya mila na desturi na kuona ni mambo yaliyopitwa na wakati. Aidha, kumejitokeza tabia hususani kwa vijana wengi kushadidia na kuiga mila na desturi za kigeni, kwa kuona ni bora zaidi kuliko za kwetu. Mila na Desturi zetu zinaonekana kuwa za kishenzi, kizamani na za aibu kwa wakati huu jambo linalosababisha jamii hususani vijana kutothamini Utamaduni wetu na kujiingiza katika vitendo vya uvunjifu wa Maadili.

### c) Mavazi yasiyositiri mwili

Ni mavazi ambayo huonesha baadhi ya viungo vya mwili au nguo za ndani, kubana sana, kutobolewa au kuchanwa na mavazi ambayo yanaacha baadhi ya sehemu za mwili wazi kama vile kiuno, kitovu, kifua. Aidha, uvaaji wa suruali au kaptula kwa mtindo wa mlegezo ambao husababisha nguo ya ndani (chupi) kuonekana haufai.Vilevile, nguo zenye mipasuo mirefu na fupi zisizofunika magoti zimekuwa ni kero katika jamii.. Ikumbukwe kuwa, mavazi yaliyotajwa hapo juu yakivaliwa mahali, tukio na wakati sahihi hayana madhara kwa kundi au walengwa waliokusudiwa.



CS CamScanner



***Picha ikionesha mavazi yasiyositiri mwili***

**d) Kukosekana kwa heshima na nidhamu kwa wakubwa**

Heshima na nidhamu vimekuwa vitu adimu sana kwa sasa hususani baina ya watoto na watu wazima. Hali hii, inajionesha katika maeneo mengi mfano katika vyombo vya usafiri, vijana hukaa kwenye viti na huku watu wazima wakiwa wamesimama. Aidha, katika mazingira ya mtaani au shughuli za kijamii, vijana wadogo wanaweza kupishana na watu wazima na wasiwasalimie, vijana na watoto kupishana na watu wazima wakiwa wamebeba mizigo bila kuwapokea. Hali kadhalika, watu wazima nao kwa sasa hukosa heshima kwa kufanya vitendo visivyofaa mbele ya watoto/vijana kama vile kutoa lugha za matusi, mavazi yasiyofaa, ulevi, uhusiano wa kingono na watoto, jambo ambalo ni kinyume kabisa na Maadili katika jamii.



CamScanner



***Picha ikionyesha ukosefu wa nidhamu na heshima kwa wakubwa ndani ya vyombo vya usafiri***

**e) Ubakaji, Unajisi, Ukatili na Ulawiti**

Tendo la kubaka hufanyika pale mwanaume anapomwingilia mwanamke au msichana kwa nguvu bila hiari (ridhaa) yake au kwa kulazimishwa au kupitia udanganyifu wa namna tofautitofauti. Kitendo hicho pia huitwa unajisi. Kulawiti ni tendo la kumwingilia mwanaume au mwanamke kinyume na maumbile (kupitia njia ya haja kubwa). Vitendo vya ubakaji na ulawiti ni makosa makubwa ya jinai na ikithibitishwa mahakamani, mhalifu anaweza kufungwa kifungo cha maisha au adhabu ya jela kwa muda mrefu. Aidha, kumekuwa na wimbi kubwa la vitendo vya ubakaji na ulawiti hapa nchini, mara nyingi tumeshuhudia vyombo vya habari vikitoa taarifa za matukio haya ya udhalilishaji ambayo hasa yanafanywa kwa watoto wadogo. Kumekuwapo na sababu mbalimbali ambazo zimesababisha kufanyika kwa matukio hayo; sababu hizo ni kama vile kuwapo kwa imani za kishirikina, matatizo ya akili na chuki katika ngazi ya familia na jamii. Athari za kufanyiwa vitendo hivi ni kubwa, huwaharibu kimaumbile na kisaikolojia waathirika na madhara yake hudumu muda wa maisha yao yote. Vitendo vya aina hii huleta chuki kubwa, uadui, uhasama na mafarakano ndani ya jamii.



CamScanner




***Picha ikionyesha mtu mzima anavyomrubuni mtoto kwa zawadi***

**Jendwali Na. 2: Matukio ya ukatili dhidi ya watoto**

| MWAKA | IDADI | | |
|---|---|---|---|
| | WANAUME | WANAWAKE | JUMLA |
| 2016 | 2,055 | 8,496 | 10,551 |
| 2017 | 3,647 | 9,810 | 13,457 |
| 2018 | 2,702 | 11,789 | 14,491 |
| 2019 | 1,214 | 7,976 | 9,190 |

**Jedwali Na. 3: Makosa ya ukatili dhidi ya watoto yaliyoongoza kwa idadi kubwa ya waathirika mwaka 2016-2018**

| Na. | 2016 | 2017 | 2018 |
|---|---|---|---|
| 1. | Ubakaji (4,423) | Ubakaji (2,984) | Ubakaji (5,557) |
| 2. | Shambulio (1,801) | Shambulio (2,752) | Mimba kwa wanafunzi (2,692) |
| 3. | Shambulio la kudhuru mwili (1,021) | Mimba kwa mwanafunzi (1,323) | Kulawiti (1,159) |
| 4. | Kujeruhi (819) | Shambulio la kudhuru mwili (1,293) | Shambulio (965) |
| 5. | | Lugha ya matusi (1,218) | Kujeruhi (705) |

### f) Ukahaba na uzinzi

Ukahaba ni mwenendo wa mwananume au mwanamke kufanya mapenzi ya kimwili na mtu yeyote kwa ajili ya kujistarehesha au biashara. Uzinzi



CamScanner

ni kitendo cha kujamiiana baina ya mwanaume na mwanamke ambao hawajaoana. Vitendo hivi hufanywa na vijana wazee na wahalifu hutumia majina tofautitofauti ili kuficha siri ya vitendo hivyo. Mfano wazee huzungumzia 'nyumba ndogo' au 'mchepuko' wakiwa na maana kuwa uhusiano huu ni nje ya ndoa. Wanawake nao hutumia maneno mengine kama 'danga', 'mshikaji', 'buzi' n.k. Vitendo kama hivi vina madhara hasi katika jamii mathalani, huweza kusababisha magonjwa ya zinaa kama UKIMWI, watoto wengi katika familia hukosa matunzo na malezi bora kutokana na mmoja wa wazazi wao kushiriki katika ukahaba na uzinzi. Madhara mengine ni ugomvi, mauaji, kuvunjika kwa ndoa na matumizi mabaya ya fedha ambazo zingetumika kuendeleza familia.



***Picha ikionyesha ukahaba na ulevi***

**g) Ushoga na usagaji**

Ushoga ni kitendo cha mwanaume kukutana kimwili (kufanya mapenzi) na mwanaume mwenzake kwa kumwingilia kupitia njia ya haja kubwa. Usagaji ni kitendo cha mwanamke kumfanyia mwanamke mwenzake vitendo vya ngono. Vitendo hivi ni vya aibu kubwa na vina kila dalili za kukufuru uumbaji wa Mwenyezi Mungu. Aidha, vitendo hivi vina athari kubwa kiafya na kiakili na vinaharibu uwezo wa kufanya kazi kwa wahusika. Siku hizi vitendo vya aina hii vimeanza kujitokeza kwa baadhi ya watu kufanya hadharani na kuweka picha katika mitandao ya kijamii. Hatuna budi kuvikemea vitendo hivi kwa nguvu zote kwani vinakinzana kabisa na misingi ya utu, miiko, Maadili na mila na desturi zetu.



CamScanner





***Picha ikionyesha  ushoga na usagaji***

### h) Malezi holela kwa watoto na vijana

Hapo za zamani, watoto na vijana walikuwa mali ya jamii nzima na hivyo kila mmoja katika jamii alikuwa na wajibu wa kuwalea na kuwaelekeza katika misingi na miiko ya mila na desturi za jamii inayohusika. Kwa sasa, kumekuwa malezi holela yenye uhuru usiokuwa na mipaka ambapo mtoto anapokiuka Maadili, hawezi kuadhibiwa na jamii kama ilivyokuwa zamani kwani familia yake inaweza kuweka uadui au ugomvi kwa yule aliyemwadhibu. Watoto na vijana wana uhuru wa kufanya lolote wanalotaka bila kuulizwa na mtu hata kama ni kinyume cha Maadili. Mfano vijana wodogo kujihusisha na vitendo vya ngono kabla ya wakati wao.

Aidha, baadhi ya wazazi kufanya vitendo vya kiutu uzima mbele za watoto kama vile kubusiana ambapo mambo hayo hutakiwa kufanyika katika eneo la faragha. Pia, wazazi kuwaruhusu watoto kuangalia picha za utupu kwenye runinga au kwa kuwanunulia simu zenye uwezo wa kuonesha mambo ya ngono na picha chafu. Hali hii inasababisha watoto kukua katika makuzi yasiyo ya Maadili mema na hivyo kuathiri maisha yao.



CamScanner

#### i) Kutokupenda kufanya kazi/uvivu

Kumeibuka tabia ya vijana ya kutopenda kufanya kazi lakini kutaka kupata maendeleo bila kujishughulisha (bila jasho). Baadhi yao wanajihusisha katika michezo ya kamari hususani michezo ya kubashiri matokeo ya mchezo wa soka na michezo mingine, kukusanyika vijiweni na kupiga soga siku nzima; n.k. Tabia hizo ni hatari kwa ustawi wa jamii kwani huchochea hali ya uvivu na tamaa ya kuwa na vitu au mali bila kufanya kazi. Mathalani, tabia ya vijana wa kiume kuwa na uhusiano wa kimapenzi na wanawake watu wazima wenye fedha nyingi kwa lengo la kufaidika na fedha hizo.



***Picha ikionyesha mimba za Utotoni***

#### j) Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya

Unywaji wa pombe kupita kiasi pamoja na utumiaji wa dawa za kulevya vinaonekana kuiathiri jamii ya sasa hususani kwa baadhi ya vijana wadogo ambao ndiyo nguvukazi ya Taifa. Matokeo ya matumizi ya vilevi hivyo kupita kiasi huleta madhara makubwa katika jamii ikiwamo ugomvi, ubakaji, ulawiti, wizi, kutukana na kuvua nguo hadharani, na matendo mengine maovu kinyume na Maadili ya jamii.

#### k) Unyanyasaji/ukatili wa Kijinsia

Jamii imekuwa ikishuhudia vitendo vya udhalilishaji na unyanyasaji wa kijinsia hususani kwa wanawake na watoto wa kike na hata unyanyasaji wa wanaume. Mfano; Mtoto wa kike anapoomba kazi hulazimika kutoa rushwa ya ngono ili kupata kazi. Aidha, kumekuwa na unyanyasaji wa mabinti na wavulana wa kazi za nyumbani. Katika tasnia za sanaa na uigizaji, mtoto wa kike akitaka kupata sehemu nzuri ya kuigiza, analazimika kutoa mwili wake kwa mwongozaji au meneja wa michezo hiyo. Matendo haya yanadhalilisha utu wa mtu na ni kinyume na Maadili ya Taifa.


CamScanner

**Jedwali Na. 4: Matukio ya ukatili wa kijinsia kwa watu wazima kuanzia mwaka 2016-2019**

| MWAKA | IDADI | | |
|---|---|---|---|
| | WANAUME | WANAWAKE | JUMLA |
| 2016 | 9,405 | 22,591 | 31,996 |
| 2017 | 13,471 | 27,945 | 41,416 |
| 2018 | 12,715 | 30,772 | 43,487 |
| 2019 | 45 | 1,205 | 1,250 |

**Jedwali Na. 5: Makosa ya ukatili wa kijinsia yaliyoongoza kwa idadi kubwa ya waathirika**

| Na. | 2016 | 2017 | 2018 |
|---|---|---|---|
| 1. | Ubakaji (7,645) | Shambulio (6,668) | Shambulio (8,822) |
| 2. | Shambulio (7,171) | Ubakaji (8,336) | Ubakaji (7,626) |
| 3. | Shambulio la kudhuru mwili (4, 565) | Shambulio la kudhuru mwili (7,219) | Shambulio la kudhuru mwili (6,397) |
| 4. | Kujeruhi (3,668) | Kujeruhi (4,661) | Kujeruhi (5,009) |

**Jedwali Na. 6: Mauaji ya wazee**

| MWAKA | IDADI | | |
|---|---|---|---|
| | WANAUME | WANAWAKE | JUMLA |
| 2015 | 80 | 102 | 190 |
| 2016 | 40 | 95 | 135 |
| 2017 | 150 | 53 | 203 |
| 2018 | 54 | 38 | 92 |
| 2019 | 29 | 45 | 74 |

## 2.2 Athari za Mmomonyoko wa Maadili

Athari za mmomonyoko wa Maadili zinaonekana katika vipengele vyake muhimu ambavyo ni Lugha, Mila na Desturi, Mavazi. Athari hizo ni kupotea kwa nguvukazi ya Taifa; kuongezeka kwa umaskini katika jamii; kudidimia kwa uchumi; kupotea kwa utambulisho asili wa mila na desturi za jamii pamoja historia; kuongezeka kwa utegemezi na uzururaji; kukithiri kwa utovu wa nidhamu; ongezeko la ujambazi na kugombea mali; kukithiri kwa vitendo vya rushwa; kuongezeka kwa mimba za utoto na zisizotarajiwa; n.k



CamScanner

### 2.2.1 Kupotea kwa nguvukazi ya Taifa

Nguvu kazi ya Taifa lolote inategemea vijana wenye afya njema, utimamu wa akili, kujitambua na kujituma kufanya kazi kwa bidii. Hata hivyo, kutokana na kuwapo kwa vitendo vya kujiingiza katika ulevi na kutumia dawa za kulevya kupita kiasi, kunasabisha vijana wengi kupoteza maisha, kupata magonjwa ya kuambukiza kama vile UKIMWI, kifua kikuu, na kupoteza uwezo wa akili na kufanya kazi na matokeo yake ni kupotea kwa nguvukazi ya Taifa.

### 2.2.2 Kuongezeka kwa umaskini katika jamii

Umaskini katika jamii hutokana na tabia ya uvivu na kutokupenda kujishughulisha na uzalishaji mali ili kujipatia kipato. Tabia hizi ni miongoni mwa mambo yanayokiuka misingi ya Maadili na matokeo yake ni kukithiri kwa umaskini ndani ya jamii. Hali ya umasikini hufanya wanajamii kuishi maisha magumu na kukosa mahitaji muhimu hususani chakula, mavazi na malazi. Wengine huishia kukaa mitaani kama ombaomba ili kuweza kujikimu.

### 2.2.3 Kudidimia kwa uchumi

Ukuaji wa uchumi unategemea namna jamii inavyojituma kufanya kazi na kuwekeza katika sekta mbalimbali za kiuchumi kama vile; Biashara, shughuli za kilimo na ufugaji; uzalishaji wa bidhaa za viwandani ikiwamo nguo, viatu, n.k; uchimbaji wa madini; uvuvi n.k., lakini pale wanajamii wanapoacha kuthamini kazi na kujihusisha na vitendo viovu kama vile kunywa pombe kupita kiasi, dawa za kulevya na uhalifu mbalimbali, husababisha kudidimia kwa uchumi wa Taifa.

### 2.2.4 Kupotea kwa historia, utambulisho asili wa Mila na Desturi za jamii

Kuwapo kwa tabia ya baadhi ya watu hususani vijana na wasomi kuiga na kupenda tamaduni za kigeni hasa za kigeni ni chanzo kikubwa cha kupotea kwa asili ya mila na desturi zetu pamoja na historia. Wengi wao wamejijengea tabia ya kuona tamaduni za kigeni ni bora zaidi kuliko za ndani ya jamii zao na hivyo kuzipuuza, kuzibeza na kutozithamini kabisa. Mathalani, mitindo ya uvaaji, uchezaji wa muziki na ulaji hufanywa kwa kufuata mila na desturi za kigeni. Kuendelea kwa tabia hii kutasababisha utambulisho wetu wa asili kupotea kwani vizazi vijavyo havitajua asili yetu ilikuwaje. Kwa mtazamo huu, jitihada za kuendeleza Utamaduni wetu zitakwama.



CamScanner

### 2.2.5 Kuongezeka kwa utegemezi na uzururaji

Kwa hivi sasa kumekuwa na ongezeko la utegemezi na uzururaji mijini na vijijini kutokana na watu kutopenda kufanya kazi na kujituma. Baadhi yao wamekimbilia mijini kutafuta kazi ilihali vijijini hakuna watu wa kufanya kazi. Aidha, kumekuwa na tabia kwa baadhi ya watoto wakubwa nyumbani wanategemea kufanyiwa kazi na wazazi wao. Jambo hili linawahusu zaidi vijana ambao wazazi wao wana kipato kizuri. Wengine wanahitaji kutafutiwa kazi na ndugu, jamaa au wafadhili wa familia jambo ambalo linaongeza hali ya utegemezi na kutokuwajibika. Sura nyingine ya utegemezi ni kukithiri kwa ombaomba kwenye Miji na Majiji makubwa hali inayodhalilisha utu na heshimu ya mtu hata kama inampatia kipato.

### 2.2.6 Kukithiri kwa utovu wa nidhamu

Suala la utovu wa nidhamu linajitokeza kwa makundi ya rika zote ndani ya jamii kuanzia kwa watoto hadi watu wazima. Kwa sasa, limekuwa jambo la kawaida kwa watoto na vijana wakiwatukana na kuwapiga watu wazima hadharani hata kama wana umri sawa na wazazi au walezi wao. Kwa upande mwingine, baadhi ya wazazi na walezi wamekosa staha na heshima ambapo wanakuwa na uhusiano wa mapenzi na watoto wao wa kuwazaa, kuwalea au hata watoto wa ndugu zao. Pia, wazazi au walezi hutumia lugha za matusi mbele ya watoto wadogo na kufanya vitendo vingine ambavyo havipaswi kuonekana hadharani.

### 2.2.7 Ongezeko la ujambazi na kugombea mali

Kwa sasa katika jamii kumekuwa na ongezeko la vitendo vya kutumia nguvu au silaha ili kujipatia mali. Vitendo vya namna hii huambatana na wizi, utapeli, uporaji, na mauaji ya watu kwa lengo la kujipatia mali au utajiri. Pia, wizi huu na utapeli umeshamiri katika mitandao. Matendo haya yanadhihirisha kiwango cha juu cha mmomonyoko wa Maadili ndani ya jamii. Kwa maneno mengine, baadhi ya wanajamii wamegeuka na kuwa kama wanyama badala ya binadamu wenye kujali utu, upendo na amani. Aidha, vitendo vya aina hii vimeongeza gharama kubwa kwa Serikali katika kuimarisha ulinzi na usalama ili kukabiliana na uhalifu huo.



CamScanner

### 2.2.8 Kukithiri kwa vitendo vya rushwa

Vitendo vya rushwa vimeendelea kuongezeka siku hadi siku ndani ya jamii. Ili kupata huduma ambazo mwananchi anastahili kupata, hutokea ukwamishwaji kwa watendaji ili kushawishi kupewa rushwa. Mathalani, watu hutoa rushwa ili kupata kazi nzuri katika ofisi fulani; matibabu ya haraka kabla ya wengine; kupewa alama za ufaulu katika mitihani; kupewa madaraka au kupandishwa cheo; kushinda kesi isivyo halali; kupata mali au utajri kwa muda mfupi; n.k. Madhara ya rushwa ni makubwa sana katika jamii kwani yanakiuka haki na ukweli. Madhara mengine ni kukosa ufanisi katika shughuli mbalimbali kwa kufanywa na watu wasio na sifa stahiki; kufunika na kuyapotezea mambo maovu; kukosa uaminifu; kuongeza hofu ndani ya jamii na hali ya wasiwasi; n.k. Hivyo, ni dhahiri kuwa kukithiri kwa vitendo vya rushwa ni sumu ya haki na maendeleo katika jamii.

### 2.2.9 Kuongezeka kwa mimba za utoto na zisizotarajiwa

Moja ya changamoto kubwa inayoikabili jamii kwa sasa ni kuongezeka kwa mimba za utotoni na zisizotarajiwa kutokana na kukithiri kwa vitendo vya ubakaji kwa watoto na vijana wadogo. Aidha, mambo haya huchangiwa na watoto wadogo kujiingiza katika uhusiano wa mapenzi katika umri mdogo. Jambo hili linaleta fedheha na taharuki ndani ya jamii kwani baadhi ya watoto wa kike hulazimika kukatisha masomo yao ili kulea mimba. Kuwapo kwa vitendo hivi ni hasara kubwa kwa jamii kutokana na kuongezeka kwa idadi kubwa ya wanafunzi wanaokatisha masomo. Aidha, jamii inatumia gharama kubwa za kuendesha maisha ya kila siku kwa kuwa na familia kubwa kinyume na matarajio au uwezo wao wa kumudu kuendesha maisha. Mbali na kuongezeka kwa mimba; madhara mengine ni kupata maambukizo ya magonjwa mbalimbali kama vile UKIMWI, homa ya ini, kaswende na kisonono na kusababisha vifo kabla ya wakati. Mimba za utotoni pia huongeza mzigo kwa familia na utegemezi uliokithiri kwani waathirika wengi hawana uwezo wa kujipatia mahitaji ya kila siku.

**Jedwali Na. 7: Mimba za utotoni**

| MWAKA | IDADI | |
|---|---|---|
| | KE | JUMLA |
| 2015 | 3,439 | 3,439 |
| 2016 | 3, 281 | 3,281 |
| 2019 | 6,237 | 6,237 |



CS CamScanner

## 2.3 Njia za kukabiliana na athari za mmomonyoko wa Maadili

Kwa kiasi kikubwa suala la Maadili limekuwa ni changamoto kwa jamii ya Kitanzania na nchi nyingi za Bara la Afrika. Hivyo, njia za kudhibiti mmomonyoko huu wa Maadili ni jukumu la kushirikisha jamii yote kutambua umuhimu, kupitia;

- Familia - Malezi
- Jamii (Watu Mashuhuri)
- Taasisi na jumuiya mbalimbali – (K.m. Shule, Asasi za dini)
- Viongozi-(katika hotuba n.k.)
- Machapisho mbalimbali – (vitabu, vipeperushi)
- Fani za utamaduni- (Sanaa, Lugha)
- Michezo
- Vyombo vya habari
- Mitandao ya kijamii

## 2.4 Mapendekezo kuhusu udhibiti wa mmomonyoko wa Maadili

Maadili ya Utamaduni wa Mtanzania yanaweza kutazamwa kwa namna tofauti kama yalivyo maisha na vipengele vyake vya kila siku. Hivyo, basi ili jamii iweze kuyaishi ni vyema kufuata misingi yake kama vile;

i) **Kudumisha Mila na Desturi**

Mila na Desturi zimebeba hazina kubwa ya Maadili ya Mtanzania na hizi zikifuatwa kikamilifu tatizo la mmomonyoko wa Maadili halitakuwapo kabisa au litapungua katika jamii.


ii) **Mavazi**

Ili Mtanzania aonekane kuwa ni mtu mwenye Maadili mema ni lazima avae mavazi yenye heshima na staha yaani yenye kusitiri mwili kulingana na umbo la mwili wake. Mtanzania yeyote hapaswi kuvaa mavazi yenye kuacha wazi baadhi ya maungo muhimu ya mwili hasa kwa wanawake na nguo za mlegezo kwa wanaume. Kwa mfano, kuna wazazi wanawaruhusu watoto wao wa kike kuvaa nguo zinazoonyesha baadhi ya sehemu za maumbile kama vile migongo, mapaja na sehemu kubwa ya kifua kuwa wazi.



CamScanner

Baadhi ya watu wazima pia hukaa vifua wazi hadharani bila kujali wanakutana na nani! Lazima tupige vita uvaaji usiokubalika katika jamii zetu ili kulinda hadhi ya utamaduni wetu kwa kizazi cha sasa na hapo baadaye.



**Picha ikionyesha vijana waliovaa mavazi ya staha na heshima**

**iii) Lugha**

Kila Mtanzania anatakiwa kutumia lugha fasaha na sanifu kwa wakati mwafaka na mazingira yanayohusika ili kulinda hadhi yake kimaadili. Lugha za kejeli, vijembe na matusi husababisha ugomvi na uvunjifu wa amani miongoni mwa wanajamii. Hivyo, matumizi ya lugha ni kipimo cha Maadili ya Mtanzania. Suala la matumizi ya lugha sahihi lipewe uzito kuanzia ngazi ya familia maana ndipo mmomonyoko wa Maadli unapoanzia zaidi kuliko mahali pengine popote.



CS CamScanner

**iv) Kufanya kazi kwa bidii na kwa ushirikiano**
Ushirikiano na kufanya kazi kwa bidii ni moja ya Maadili mahimu ya Mtanzania. Hali hii hujidhihirisha katika shughuli za kijamii kama vile; Ujenzi wa miundombinu mbalimbali mfano; shule, barabara, hospitali, misiba na sherehe.

**v) Ukarimu, upendo, heshima na nidhamu**
Ukarimu, upendo, heshima na nidhamu ni msingi mkubwa wa Maadili ya Mtanzania kwani mtu akiwa mkarimu, mwenye upendo, heshima, nidhamu na tabia njema hawezi kabisa kwenda kinyume na Maadili. Kama Watanzania tuna wajibu wa kupendana, kuheshimiana, na kukirimiana ili kuondoa chuki, ubinafsi ambao kwa kiasi kikubwa husababisha rushwa, ugomvi, ukosefu wa amani, na kurudisha nyuma maendeleo ya nchi yetu.

## 2.5 Hitimisho la Sura ya Pili

Katika sura hii tumetazama kwa kina hali ya mmomonyoko wa Maadili jinsi ulivyo nchini. Tumejaribu kuangazia viashirio vya mmomonyoko wa Maadili, athari za kuongezeka kwa utomvu wa Maadili kijamii na kiuchumi. Tunapenda kueleza kwa uwazi kuwa, jamii legelege isiyokuwa na Maadili huzaa taifa legelege. Taasisi zote kama shule, dini, jamii, familia, vyombo vya usalama n.k, zinazoweza kuhakikisha wanazaliwa vijana wa Kitanzania wenye Maadili sahihi zitimize wajibu wake katika kutmiza azima hiyo.



CS CamScanner

# SURA YA TATU
# WAJIBU KWA MAKUNDI MBALIMBALI KATIKA KUKUZA NA KUENDELEZA MAADILI NA UTAMADUNI

## 3.0 Utangulizi

Jukumu la kuendeleza Mila, Desturi na Utamaduni wetu ni la kila mmoja katika jamii kwani ndicho kichocheo muhimu cha uzalendo uliopo hususani katika suala zima la Maadili.Thamani ya utamaduni mara nyingi imekuwa ikionekana kwenye sekta nyingi kama elimu, afya, michezo, kilimo, utalii, viwanda na maendeleo ya jamii, ambapo wadau wote ikiwa ni pamoja na sekta binafsi na wananchi kwa ujumla wanatakiwa washirikiane katika kulinda, kutunza, kutangaza na kuendeleza Utamaduni na Maadili ya Mtanzania. Katika kuhakikisha Utamaduni na Maadili ya Mtanzania yanazingatiwa yapo makundi kadhaa kama Serikali na taasisi zake, Sekta Binafsi na jamii ambao wana wajibu wa kukuza na kuendeleza Maadili yetu.

## 3.1 Wajibu wa familia

Kwa kawaida mafunzo ya Maadili yanaanzia katika familia yaani kutoka kwa baba na mama au mlezi na kuendelea hadi ngazi ya shule. Aidha sehemu nyingine ni za makazi hadi ngazi ya Taifa, lakini wazazi au walezi wasipotimiza wajibu wao wa kuwafundisha Maadili watoto wao mapema, watoto au vijana hao kwa sababu wana akili watajifunza na kuiga jambo lolote linalowafurahisha kutoka maeneo ya shule au popote katika makazi yao, ndani au hata nje ya nchi. Suala la kulea au malezi ya watoto na vijana katika jamii ni jukumu la jamii nzima ingawa siku hizi jukumu hili limeachiwa wazazi/walezi wa familia ambayo mtoto au kijana anatoka. Kuachwa kwa suala la malezi shirikishi katika jamii zetu za Kitanzania kumesababisha watoto na vijana wetu kukosa Maadili na hivyo kusababisha kumomonyoka kwa Maadili mema katika jamii zetu. Jambo la kusisitiza hapa ni kwamba, suala la malezi ya watoto na vijana wetu liwe ni jukumu letu sote na siyo vyema kuwaachia familia husika tu, na kwamba jamii zetu zikiwa na tabia na mienendo isiyokubalika ni dhahiri kuwa matokeo yake yataiathiri jamii nzima. Ni wajibu wa kila Mtanzania kutambua umuhimu wa malezi kwa watoto na vijana. Vivyo hivyo, walezi/wazazi wanahimizwa kuishi kiuadilifu ili kuchochea Maadili kwa watoto na vijana kwa faida ya Taifa.



CamScanner

## 3.2 Wajibu wa Serikali

### a) Viongozi wa Umma

Serikali kwa kuona umuhimu wa Maadili kwa viongozi wa umma ilianzisha chombo kinachosimamia tabia na Maadili ya viongozi wa umma. Chombo hicho ni Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa umma kilichoanzishwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 ibara ya 132 na Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Na. 13 ya mwaka 1995 (Sura 398).

Vilevile, suala la Maadili linaweza kusimamiwa na viongozi wa Serikali za mitaa, vitongoji na vijiji. Katika utendaji wake wa kazi Serikali za Mitaa zina kamati za Maadili ambazo kazi yake ni Kusimamia Maadili na masuala mbalimbali yanayohusu nidhamu pamoja na mashauri mbalimbali, kutoa ushauri na maelekezo kuhusu kanuni, Sheria na taratibu zilizopo, Kuhimiza jamii kufanya kazi kwa bidii, kujituma na kuimarisha ushirikiano miongoni mwa jamii, kukemea vitendo viovu katika maeneo wanayosimamia kama vile ulevi, matumizi ya dawa za kulevya, ujambazi na wizi, uporaji na uzururaji; Kusisitiza mshikamano, upendo, umoja na amani kupitia mikutano ya uongozi wa kijiji au mtaa.

Hivyo, katika kusimamia Maadili yaliyoainishwa katika kanuni na sheria zilizoainishwa hapo juu, inatarajiwa viongozi wa umma kwa ngazi zote watatekeleza wajibu ufuatao:-

- Kulinda na kuhifadhi mila na desturi za Mtanzania
- Wao binafsi kuishi kiadilifu hususani katika mavazi yao, lugha yao, maelekezo wanayoyatoa na mienendo yao kwa ujumla.
- Kusimamia Maadili kwa watu walio chini yao.

### b) Wizara, Idara na Taasisi za Kiserikali

Katika kukuza na kuendeleza utamaduni na Maadili katika jamii Serikali kupitia Wizara, Idara na taasisi za mbalimbali zinahimiza ukuzaji wa Maadili kwa umma. Kwa mfano, iliyokuwa Wizara ya Utamaduni Habari, Sanaa na Michezo kwa wakati huo, ambapo kwa sasa ni Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo nchini iliunda Taasisi ambazo zina majukumu ya kusimamia utamaduni na Maadili ya Kitanzania. Taasisi hizo ni Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA); Bodi ya Ukaguzi wa Filamu na Michezo ya Kuigiza (BFT); Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa); Baraza la Michezo la Taifa (BMT); Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA). Wizara ya mambo ya ndani



CamScanner

imepewa jukumu la kusimamia na kutekeleza Sheria zinazosimamia watu katika Maadili. Kwa mfano, inapotokea uvunjifu wa Sheria, polisi hutumia Sheria na kanuni za nchi kumfikisha mhusika Mahakamani, hatimaye akithibitkika kuwa na hatia hupelekwa gerezani ili kurekebisha tabia na mwenendo wa mhusika ili aweze kukubalika tena na jamii.

Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa pia inazo taasisi zake kama Jeshi la kujenga Taifa (JKT), na Jeshi la Wananchi (JWTZ) ili kuimarisha na kusimamia Maadili kwa umma. Wizara ya Sheria na Katiba kupitia Mahakama na Bunge hutunga na kusimamia utekelezaji wa Sheria za nchi ili kukuza Maadili kwa umma. Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto kupitia Idara ya Ustawi wa Jamii pia inasimamia na kutekeleza usimamizi wa Maadili ya taifa kupitia Kitengo cha Familia na Watoto katika kusimamia malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya watoto wadogo. Kupitia mifano hiyo michache, wizara na taasisi zake zina wajibu mkubwa wa kusimamaia mila, tamaduni na desturi za Mtanzania kwa ajili ya kujenga umoja na mshikamano wa kitaifa kwa ustawi wa wananchi wake. Hivyo, mwongozo huu unahimiza;

- Usimamizi madhubuti wa Sheria, taratibu na kanuni katika kusimamia Maadili Nchini kupitia Wizara, Idara na taasisi zake.
- Pamoja na wajibu waliopewa Wizara, taasisi na idara za serikali, zisisitizwe utekelezaji wa Mwongozo unaozitaka taasisi zote za umma kuwa na kamati za Maadili mahala pa kazi.

### c) Taasisi za Elimu

Taasisi za elimu zina majukumu ya kufundisha Utamaduni na MMaadili ya Kitanzania kuanzia ngazi ya Shule ya Awali mpaka ngazi ya Elimu ya Juu. Katika mitaala ya elimu kwa ngazi zote kumewekwa mkazo katika kujenga uelewa na kuendeleza Utamaduni na Maadili.

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 13 ya Mwaka 1975. Pamoja na majukumu mengine TET ina majukumu ya kutafsiri kwa vitendo Sera mbalimbali za Serikali katika programu za elimu na mitaala inayowezesha utoaji wa elimu bora kuanzia elimu ya awali, msingi, sekondari na vyuo vya ualimu. Katika programu zake za elimu na mitaala wanafundisha masuala ya Utamaduni na Maadili. Kwa hivyo;

- Ni wajibu wa Taasisi za elimu kuona haja ya kuweka misingi imara katika kulea, kuimarisha ubora wa vijana ili kufikia kiwango cha ubora kinachokubalika katika jamii.



CamScanner

- Vijana na watoto au watu wengine walio katika taasisi hizi za elimu lazima wawe katika ubora wa Maadili. Wajibu wa taasisi za elimu ya juu iwe ni
- Kuandaa na kuboresha mikakati yao ili kupata wataalamu wanaokidhi vigezo vya uadilifu.

## 3.3 Wajibu wa Sekta binafsi

Sekta binafsi ni miongoni mwa wadau wanaoshiriki katika kukuza na kuendeleza Utamaduni na MMaadili ya Mtanzania. Sekta hii imekuwa ikiwekeza, kufadhili, kuandaa na kuendesha mashindano ya maonesho mbalimbali ya michezo, sanaa na burudani. Mfano katika Ligi kuu ya Mpira wa Miguu ya Tanzania (VPL VODACOM), Matamasha ya Sanaa na Utamaduni kama vile; JAMAFEST, Sinema zetu (AZAM MEDIA) na Sauti za Busara. Sekta hii ina mchango wa kuhakikisha Maadili ya Kitanzania yanasimamiwa ipasavyo. Kwa maelekezo na umuhimu wao, inatakiwa;

- Kwenye kila sekta binafsi ianzishe Kamati ya Maadili inayohusika na sekta hiyo kwa ajili ya kusimamia tabia na mienendo katika utekelezaji wa majukumu yao.
- Kamati hizi zisimamie uendeshaji wa shughuli zake za kila siku katika jamii kwa kuzingatia Maadili (tabia na mwenendo mwema). Vilevile iwajibike kuwasilisha taarifa kwa wizara inayohusika.

## 3.4 Wajibu wa makundi ya jamii

**i) Viongozi wa Dini**

Viongozi wa dini wana majukumu yaa kuimarisha malezi na mafundisho ya kiroho kwa jamii hususani vijana ili kuwaepusha na mmomonyoko wa MMaadili na wawe na utu wema ili jamii iendelee kung'ara, kuheshimika na kusifika kwa utulivu, amani, umoja na mshikamano wa kitaifa. Viongozi hao wana nafasi kubwa ya kutengeneza mustakabali mwema na ustawi wa mtu mmojammoja, familia na makundi mbalimbali kupitia mahubiri/mawaidha na kutoa habari njema na malezi ya kiroho kwa waumini wao katika kujenga familia imara na thabiti yenye hofu ya Mungu. Hivyo;

- Ni wajibu wa kila kiongozi wa dini kuzingatia Sheria, Miongozo na Taratibu za nchi zilizoanzisha taasisi ya dini husika.



CS CamScanner

ii) **Viongozi wa kimila**

Hili ni kundi muhimu katika kukuza na kusimamia MMaadili. Kundi hili kwa kawaida huwa na kazi ya kulinda miiko na desturi za jamii inayohusika. Kundi hili linategemewa kuwa chachu ya usimamizi wa Maadili katika kuongoza, kutoa maelekezo na mafunzo ya Maadili katika jamii zao. Hivyo, katika utekelezaji wa Maadili kundi hili lina uwezo wa kulinda hadhi na Maadili ya Taifa. Kwa hiyvo;

- Katika kutekeleza majukumu yao wanapaswa wazingatie Sheria za nchi ili kuepuka kukinzana baina ya mila, desturi na sheria zilizopo.

iii) **Wasanii**

Wasanii ni kundi muhimu ambalo lina nafasi kubwa katika kujenga Utamaduni na Maadili kupitia kazi za sanaa mbalimbali zenye mwelekeo wa kuhabarisha, kuburudisha na kuelimisha jamii ili kujenga umoja,mshikamano na upendo ndani ya jamii husika pamoja na kuenzi Maadili ya Taifa;

- Wasanii kama kioo cha jamii wana wajibu wa kujenga taswira na haiba inayokubalika kiMaadili na kiutamaduni kupitia kazi za sanaa wanazozifanya.
- Wasanii wanahimizwa kutengeneza, kuzalisha na kuwasilisha kazi zao katika maudhui yanayozingatia utamaduni na Maadilii ya Kitanzania.




***Picha ikionyesha wasanii walivyo na wajibu wa kuifikishia jamii ujumbe kuhusu Maadili***



CamScanner

iv) **Wanahabari**

Kundi hili lina nafasi kubwa katika kushiriki kujenga Uzalendo, Maadili, na Utamaduni wa nchi, pamoja na kuelimisha, kuibua na kufichua vitendo vinavyohatarisha Utamaduni na Maadili. Wanahabari wakitumia kalamu na sauti zao vyema, wanaweza kujenga na kuimarisha misingi ya Utamaduni na Maadili lakini wasipozitumia vyema, huweza kuhatarisha, kubomoa Maadili na Utamaduni wa Mtanzania. Mathalani, jamii imeshuhudia matumizi mabaya katika baadhi ya mitandao ya kijamii kama vile; facebook, Instagram, Twitter, youtube, whatsapp, ambayo hupendwa na kutumiwa na vijana wengi zaidi. Kutokana na kutozingatia matumizi sahihi ya mitandao hiyo, watumiaji wamekuwa huru kuitumia na kuiga tamaduni za kigeni zinazokinzana na Utamaduni na Maadili ya Mtanzania. Hivyo basi;

- Wanahabari wana wajibu mkubwa wa kulinda, kuheshimu na kuzingatia misingi ya kitaaluma kama yalivyoainishwa katika miongozo ya taaluma zao.
- Wanahabari wazingatie Maadili ili wananchi wajenge heshima na imani dhidi yao na kushiriki kikamilifu katika kujenga na kulinda Utamaduni na Maadili ya Mtanzania.

v) **Asasi za Kiraia**

Kundi hili linatakiwa kushirikiana na serikali na jamii kwa ujumla katika kuibua, kukemea na kufichua vitendo ambavyo vinakiuka Maadili na Utamaduni wa Mtanzania. Kundi hili lina wajibu wa kuhamasisha na kuelimisha jamii katika kujenga misingi ya Maadili na kulinda utamaduni wa Mtanzania. Hata hivyo, jamii imekuwa ikishuhudia baadhi ya Asasi za Kiraia zikishabikia baadhi ya mambo yanayozuiliwa na Serikali ambayo ni kinyume na Maadili mfano; mapenzi ya jinsia moja, upotoshwaji wa baadhi ya vyombo vya habari na ndoa za utotoni. Asasi za kiraia zinasisitizwa;

- Kuheshimu katiba ya nchi ili kulinda Maadili na Utamaduni wa Watanzania.
- Kuzingatia sheria zinazounda asasi inayohusika.

vi) **Bodi za Kitaaluma (Mfano, Bodi za wakandarasi, madaktari, wahasibu,)**

Bodi hizi zina majukumu ya kusimamia misingi ya utii wa taaluma mbalimbali ili kuwawezesha wahusika kudumisha miiko na misingi ya taaluma zao kwa lengo la kuleta ufanisi wa majukumu ya kazi zao. Hata hivyo, imebainika kuwapo kwa ukiukwaji wa Maadili kwa baadhi ya wanataaluma. Hivyo;

- Ni wajibu wa kila mwanataaluma kuzingatia misingi ya uadilifu inayohusiana na taaluma yake.
- Bodi za Kitaaluma zina wajibu wa kuhimiza, kukuza, kuendeleza na kusimamia Maadili ya Kitaaluma ili kuleta tija katika utendaji wao.
- Aidha, Bodi za Kitaaluma ziwajibike katika kuchuka hatua za kinidhamu pale inapothibitika kuwapo kwa ukiukwaji wa Maadili ya Kitaaluma.

## 3.5 Hitimisho la Sura ya Tatu

Katika sura hii tumebainisha wajibu wa makundi mbalimbali katika kukuza na kuendeleza Maadili na Utamaduni wa Mtanzania. Ni ukweli usiopingika kuwa jukumu la kulinda na kuendeleza Maadili na Utamaduni wetu ni la kila mwananchi. Aidha, makundi mbalimbali kama vile; Viongozi wa Dini, taasisi za Elimu, Asasi za Kirai, Wasanii, Wanahabari, Viongozi wa Kimila na Bodi za kitaaluma wana wajibu wa kuhakikisha Maadili na Utamaduni wetu unalindwa na kuendelezwa ili kujenga amani, upendo, umoja na mshikamano katika jamii.



CamScanner

# SURA YA NNE
# USIMAMIZI, UHIFADHI, UKUZAJI NA UENDELEZAJI WA MAADILI NA UTAMADUNI

Katika kusimamia Maadili ya Jamii ya Watanzania, kila mmoja anapaswa kuona umuhimu wa suala hili na kujichukulia kama sehemu yake. Tunapaswa kusimamia, kutunza na kuhifadhi Maadili sahihi kwa jamii yetu. Tanzania iwe nchi ya mfano wa kuzungumziwa na kila mmoja katika dunia yetu.

## 4.0 Usimamizi wa Maadili

Kuishi kwa kuzingatia Maadili, Miiko na Utamaduni wa jamii husika ni jambo muhimu sana. Miongoni mwa masuala yanayotakiwa kupewa kipaumbele katika kuyasimamia na kuyahifadhi, kuyakuza na kuyaendeleza kwa nguvu zote ni Maadili. Aidha, ikumbukwe kuwa jukumu la kuishi kwa kuzingatia Maadili na Utamaduni wetu linamgusa kila mmoja katika jamii na siyo la Serikali tu.

Mmomonyoko wa Maadili tunaoushuhudia leo ni matokeo ya kasumba iliyojengeka katika jamii ya kuamini kuwa Serikali pekee ndiyo yenye jukumu la kusimamia na kulinda Maadili na Utamaduni wetu.

Ni wajibu wa kila mwanajamii kuhakikisha kwamba analinda, anaheshimu na kuishi kwa kuzingatia Maadili hususani kwa kuanzia ngazi ya familia ambayo ndiyo chimbuko la jamii. Mathalani ni rahisi kuonyana na kurekebishana katika familia kwa minajili ya kuwasaidia watoto na vijana kwa kuzingatia Maadili na miiko inayokubalika ndani ya jamii. Mfano katika familia ni rahisi kujifunza kuheshimu wakubwa na wadogo, kusalimia, kufanya kazi kwa bidii, kuepuka lugha za matusi na kuepuka ugomvi, n.k.

## 4.1 Njia za usimamizi, uhifadhi, ukuzaji na uendelezaji Maadili na Utamaduni wa Mtanzania

Ili tuweze kuwa na Maadili endelevu ambayo tutayarithisha vizazi kwa vizazi katika jamii yetu ya Watanzania, tunapaswa kusimamia na kutekeleza mambo muhimu yafuatayo;



CS CamScanner

### 4.1.1 Kuandaa na kuendesha vipindi katika Vyombo vya Habari

Vyombo vya habari ni nyenzo muhimu sana katika kufikisha ujumbe kwa jamii kwa kuwa vina uwezo wa kuwafikia watu wengi kwa wakati mmoja. Tanzania inakadiriwa kuwa na watu zaidi ya milioni hamsini (50) na hivyo si jambo rahisi kuwafikia wote kwa haraka. Katika kuhakikisha jamii inakumbushwa na kuhimizwa umuhimu wa kuzingatia Maadili, kuwapo na vipindi vya mara kwa mara katika vyombo vya habari (Redio na Televisheni) vitakavyotoa elimu kuhusu masuala mbalimbali yaliyoainishwa katika Mwongozo huu kwa lengo la kukuza uelewa kwa jamii. Aidha, makala mbalimbali zitaandaliwa na kutolewa kwenye magazeti mbalimbali hapa nchini yakielezea umuhimu wa kuzingatia Maadili na Utamaduni wetu.

### 4.1.2 Kufanya vikao, mijadala na makongamano na wadau wa aadili na Utamaduni

Katika kujenga uelewa mpana zaidi kwa wananchi, kutafanyika vikao, mijadala na makongamano kwa kushirikiana na wadau wa utamaduni ambapo suala la Maadili litajadiliwa kwa kina na kutiliwa mkazo.

### 4.1.3 Kusambaza Mwongozo wa Maadili na Utamaduni wa Mtanzania

Mwongozo huu utasambazwa kwa wadau mbalimbali zikiwamo Taasisi za Elimu; Sekta Binafsi; Asasi za Kiraia na makundi mengine ya jamii ili kuhakikisha maudhui ya Mwongozo huu yanawafikia na kuwanufaisha watu wengi. Usambazaji utafanywa kwa kutumia majukwaa mbalimbali.



***Picha ikionyesha usambazaji wa Mwongozo wa Maadili kwa watu mbalimbali***



CamScanner

### 4.1.4 Kuandaa programu za utoaji elimu kwa umma kupitia mitandao ya kijamii

Programu za elimu kuhusu Maadili na Utamaduni zitaandaliwa na kuingizwa katika Mitandao ya Kijamii kama vile *Twiter, Instagram, Whatsapp, Facebook na Youtube* ambapo kundi kubwa la vijana hutumia muda mwingi kuperuzi na kupakua maudhui.

### 4.1.5 Kufanya tathimini endelevu

Tathimini endelevu inapaswa kufanywa kila baada ya muda ili kuona haja ya mabadiliko yaliyopo na kuona umuhimu wa kufanya mabadiliko yanayoendana na dunia iliyopo lakini katika namna ya kuenzi Maadili yetu. Hii inaweza kufanyika kupitia hojaji ambazo zitaandaliwa na kusambazwa ili kutathimini namna tunavyopiga hatua katika kudumisha na kulinda utamaduni na Maadili yetu. Hojaji hizi zitawasilishwa katika mikoa na halmashauri zote kupitia kwa Maofisa Utamaduni wa maeneo yanayohusika.

## 4.2 Hitimisho la Sura ya Nne

Tusisubiri kuelekezwa na mtu yeyote, kila mmoja katika nafasi yake anatakiwa kutimiza wajibu wa kulinda, kutetea na kuendeleza Maadili na Utamaduni wetu. Kama jamii ya Watanzania, hatuna budi kuwa wazalendo kwa nchi yetu kwa kulinda na kuendeleza Maadili, Mila, Desturi na lugha zetu.



CamScanner

# SURA YA TANO
# MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KATIKA KULINDA, KUKUZA NA KUENDELEZA MAADILI NA UTAMADUNI WA MTANZANIA


Katika kufikia lengo letu la pamoja, kila mtu kuanzia mtu mmoja, familia, jamii na taasisi za umma tuna wajibu wa kutekeleza majukumu yetu kama yalivyoainishwa ili kutunza Maadili yetu. Katika sura hii, tumejadili na kutoa mapendekezo ya kuzingatiwa na watu wa kada tofauti ndani ya nchi wakiwamo hawa wafuatao;

## 5.0 Wazazi/ Walezi kuwa mfano bora katika Familia

Wazazi wa karne hii wengi wanawalaumu watoto/vijana kuwa wana MMaadili mabaya, lakini chanzo cha tatizo hili ni wao wenyewe. Baadhi ya wazazi wamekuwa wakilewa, kutukanana, kupigana au hata kufanya mambo mengine machafu kama vile uzinzi mbele ya watoto. Kwa hakika, tabia hizi zinapofanywa mbele ya watoto nao huziiga na kuzifanya. Wazazi wengine pia wamekuwa wakiwadekeza au kutosimamia vyema Maadili kwa watoto wao na kuwafanya kukua bila malezi bora. Hivyo, wazazi wachukue jukumu la kuwa walimu wa watoto na vijana na kuwafundisha mienendo inayokubalika katika jamii, vilevile, kila mtu mwenye umri mkubwa awe mfano wa kuigwa kwa wale wenye umri mdogo kwa kuonesha tabia njema, heshima, na mwongozo sahihi wa matendo yanayofaa kutendwa na kila mwanajamii.



CamScanner



***Picha ikionyesha wazazi wakizungumza na watoto wao kuhusu Maadili mema***

## 5.1 Matumizi sahihi ya teknolojia

Teknolojia ina manufaa yake lakini pia ina hasara zake hasa kwenye malezi ya watoto na uhuru wa matumizi ya teknolojia umekuwa mkubwa. Leo hii, watoto wanatazama mambo maovu kwenye televisheni na mtandao wa intaneti na kuyaiga. Jambo hili limesababisha watoto kujifunza tabia chafu kutoka kwenye tamaduni za kigeni zilizoporomoka Maadili. Hata hivyo, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inapaswa iweke mipaka na matumizi sahihi ya Teknolojia.



CamScanner



***Picha ikionyesha watoto wakijifunza Maadili na Utamaduni kwa njia ya Mtandao***

## 5.2 Kila Mtu Kujenga Utamaduni wa Uwajibikaji

Uhai wa jamii yoyote ile hujidhihirisha kupitia matunda ya jitihada za jamii husika katika uzalishaji mali na ubunifu wa nyenzo mpya za kimaendeleo kadiri ya utaratibu uliowekwa.

Hivyo ni muhimu jamii nzima kuwajibika katika kazi binafsi na za umma ili kujipatia kipato halali kwa kuzingatia na kutii sheria na kanuni mbalimbali zilizowekwa na jamii na kuhakikisha kuwa:.

- Kila Nyanja inawaajibika katika jamii ili kutekeleza suala la Maadili
- Wanafunzi wanafundishwa somo la Maadili shuleni
- Taifa linakuwa na wabobezi wa masuala ya Maadili
- Zinaundwa klabu mbalimbali zitakazokuwa zinaelezea masuala ya Maadili katika makundi mbalimbali ya jamii
- Suala la Maadili lipewe uzito katika jamii (Mfano katika vikao vya madiwani au shuleni.
- Uwajibikaji katika jamii unakweenda sambamba na Maadili



CamScanner

## 5.3 Kukemea upotofu wowote wa Maadili unaoibuka katika jamii

Kwa nguvu na sauti moja, jamii nzima ipinge na kukemea mapokeo ya tamaduni za kigeni zinazopotosha jamii, mathalani, ushoga, usagaji, ndoa za jinsi moja, matumizi ya dawa za kulevya, uvaaji usiokubalika. Ni mambo ambayo yanatakiwa kukemewa kwa nguvu zote. Vilevile,

- viongozi wa dini, serikali na jamii kwa pamoja wasimamie misingi ya Maadili.
- viongozi wa ngazi zote wa makundi mbalimbali ya jamii wakemee vikali vitendo vya upotofu wa Maadili.

## 5.4 Kuheshimu imani za kidini

Dini zina nafasi kubwa katika kuadilisha jamii kupitia mahubiri na tafsiri ya vitabu na miongozo ya kidini. Mathalani, kutekeleza amri kumi za Mungu katika Biblia huelekeza namna ya kuepuka maovu na kutenda yanayopaswa kufanywa ikiwamo tabia na mwenendo mwema. Hivyo, ni muhimu kila mwanajamii kwa kadiri ya imani yake kuheshimu imani hizi ambazo kimsingi ni mwongozo wa mienendo inayokubalika. Pia, viongozi wa kiroho wanatakiwa kufuata maandiko yaliyopo katika miongozo yao.



***Picha ikionyesha familia ikisali***

## 5.5 Kuwa na marafiki wema

Inawezekana mtoto amelelewa vizuri nyumbani lakini akajifunza mambo mabaya kutoka kwa marafiki zake. Jambo hili limesababisha Maadili ya watoto kuharibika kwani watoto wanaotoka katika familia au mazingira yenye kiwango kikubwa cha kuporomoka kwa Maadili huwafundisha wengine tabia mbaya. Hata hivyo, elimu iendelee kutolewa katika ngazi ya familia ili watoto waendelee kujitambua.



***Picha ikionyesha mtoto akimsalimia mkubwa***



CamScanner

## 5.6 Kuepuka masuala ya unyanyasaji

Vitendo vya unyanyasaji vimeshamiri sana leo hii. Watoto, wafanyakazi wa nyumbani huchomwa, hupigwa sana, hubakwa, hulawitiwa na hata kufanyiwa unyanyasaji mwingine. Matendo haya yanaweza kumharibu mtoto kisaikolojia na kumfanya akue akiwa na majeraha ya nafsi na akili ambayo humfanya awe na tabia mbaya. Mara nyingi watoto waliofanyiwa unyanyasaji hutaka kulipa kisasi au hukata tamaa na kuishi maisha ya hovyo. Vilevile, jamii iangalie zaidi chanzo cha tatizo na kutoa ushauri kwa waathiriwa badala ya kundelea kuwalaumu ili tatizo lisiendelee.

## 5.7 Hitimisho la Sura ya Tano

Jukumu la kuendeleza Utamaduni na Maadili ya Mtanzania ni la watu wote katika ngazi mbalimbali za jamii. Viongozi na wananchi katika maeneo yao wana wajibu wa kuhamasisisha jamii kuthamini, kujivunia na kuenzi utumaduni wetu badala ya kubeza na kutekeleza baadhi ya mipango ya kukuza Utamaduni na Maadili inayobuniwa na Serikali. Makundi yote ya jamii yashiriki kikamilifu katika juhudi za pamoja za kukuza na kujenga Utamaduni na Maadili ili kurithisha kwa kizazi kijacho malezi bora na utu wema.

Aidha, ikumbukwe kwamba majukumu ya Serikali ni kuweka miongozo, kuratibu na kusimamia uendeshaji wa shughuli za Utamaduni. Kimsingi, Utamaduni unaendeshwa na wananchi wenyewe hivyo, wasimamizi wa ngazi mbalimbali kuanzia ngazi ya kaya huelimishwa ili kila mmoja ashiriki kikamilifu katika majukumu haya. Kama inavyofahamika, Utamaduni ni alama/utambulisho wa Taifa husika kwa hiyo hakuna anayetamani kuwa na alama mbaya. Taifa la Tanzainia linapaswa kusimamia misingi imara ya Maadili ili kudumisha Utaifa wetu. Ushiriki wa jamii nzima katika majukumu haya utaleta ufanisi katika utekelezaji wa mikakati na hivyo, kuleta umoja, mshikamano na uzalendo, hatimaye kuchochea maendeleo katika nyanja zote.



CS CamScanner

# MAREJELEO


1. Wizara ya Elimu na Utamaduni: *Sera ya Utamaduni ya mwaka 1997*
2. Daniel K. Ndagala: *Utamaduni na Maendeleo nchini Tanzania mwaka 2018*
3. Umoja wa Wazazi: *Kuporomoka kwa Maadili mwaka 1998*
4. Wizara ya Utamaduni wa Taifa na Vijana: *Cultural Revolution 1962*




CamScanner

# NOTSI



CamScanner